




**Kibano** chaja mapato kiduchu kwa halmashauri

UKURASA 3



**LEWANDOWSKI ATHIBITISHA KUONDOKA BAYERN**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumatatu Mei 16, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580947

www.ippmedia.com

Th[illegible]n digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




# Mchechu adai bil. 3/- fidia madai kuchafuliwa

UKURASA 2



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilbrod Mutafungwa, akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufanya ukaguzi wa magari ya abiria na mizigo yaendayo mikoani ikiwa ni operesheni ya kudhibiti na kuzuia ajali za barabarani, juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

## Wadau, watumishi wapongeza kupanda viwango mishahara

UKURASA 2

MAKALA MAALUM

## Royal Tour na fursa lukuki uwekezaji mkoani Dodoma

UKURASA 4

**MICHEZO** **PABLO: YANGA HAIKUSTAHILI FA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, akizungumza na wajumbe 750 wa Klabu ya Rotary kutoka Tanzania, Uganda, Nigeria, New Zealand, Poland na Afrika Kusini katika mkutano wa 97 wa kimataifa wa Klabu ya Rotary uliofanyika jijini Arusha mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Kiongozi wa Klabu ya Rotary Kanda ya Moshi, Young Kimaro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mchechu adai fidia bil. 3/- madai kuchafuliwa

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Nehemiah Mchechu, amefungua kesi katika Mahakama Kuu ya Tanzania, akiombwa kulipwa fidia ya Sh. bilioni tatu na gazeti la The Citizen kwa madai ya kuandika habari zilizomchafua na kumshushia hadhi kitaifa na kimataifa.

Kesi hiyo ilianza kusikilizwa Ijumaa iliyopita jijini Dar es Salaam mbele ya Jaji Leila Mgonya wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam. Katika kesi hiyo, Mchechu anawakilishwa na mawakili wa kujitegemea Aliko Mwamanenge ma Vitalis Peter.

Mchechu anadai kuwa gazeti hilo katika toleo lake la Machi 23, 2018, lilichapisha habari yenye kichwa kinachosomeka 'Why JPM dissolved NHC Board, sacked Mchechu', kwa tafsiri isiyo rasmi 'Kwa nini JPM (John Magufuli- aliyekuwa Rais) alivunja Bodi ya NHC, kumfukuza Mchechu'.

"Machi 23, 2018 ilikuwa siku ya kiza kwangu. Ni siku ambayo niliandikwa na gazeti la the Citizen ukurasa wa mbele habari ambayo ililenga kunichafua, kunishushia hadhi, kunikosanisha na jamii kubwa ya Watanzania na kuonekana kuwa ni mtu nisiyefaa kabisa kuwa kiongozi au sehemu ya jamii njema ya Watanzania. Mtu nisiye na maadili, nisiyeaminika na kimsingi nisiyestahili hata kuongoza popote," alidai Mchechu alipoongozwa na Wakili Peter katika kutoa ushahidi wake.

Mchechu ambaye alirejeshwa katika nafasi hiyo miezi kadhaa iliyopita na Rais Samia Suluhu Hassan baada ya kuondoka mwaka 2018, alidai kwamba habari hiyo ina upotoshaji mkubwa kimantiki na kimaudhui kwa kuwa hajawahi kufukuzwa kazi kama ilivyodaiwa.

"Gazeti hili liliandika habari likijua sijafukuzwa, kwa kuwa sijafukuzwa kazi na wala Mheshimiwa Rais hakuwa na hakuwahi kunifukuza kazi. Kwa hiyo hii ilikuwa habari ya uongo na yenye nia ovu ya kunichafua na kunishushia hadhi yangu katika familia yangu, taifa na duniani kwa ujumla," alidai.

**CHANZO CHA MADAI**

Katika habari hiyo iliyobeba habari kubwa ukurasa wa mbele ya kuwekwa ukurasa wa nne, ilidaiwa kuwa Mchechu alikuwa akichunguzwa na Bodi ya NHC na kuhojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) juu ya mgongano wa kimaslahi juu ya utafutaji na upatikanaji wa ekari 500 za mradi wa NHC wa Safari City jijini Arusha.

Ilidaiwa kuwa ardhi hiyo, awali iliripotiwa kununuliwa na kampuni inayomilikiwa na Mchechu ambayo iliinunua kutoka kwa raia wa kigeni na uchunguzi ulionyesha kuwa aliiuzia NHC kwa bei ya juu.

Pia kwa mujibu wa habari hiyo, Mchechu alidaiwa kumtumia mkandarasi wa NHC kutengeneza barabara kwenda kwenye eneo lake lililo karibu na eneo la mradi wa Safari City huku gharama zikiwa zinabebwa na shirika.

Sambamba na hayo, taarifa hiyo ilidai kuwa kampuni ya PHILS International ya Dubai ilipewa kazi katika mradi wa Kawe kwa uamuzi wa Mchechu bila kumhusisha Mkuu wa Kitengo cha Ununuzi cha NHC, Hamis Mpinda.

Aidha, habari hiyo ilidai kuwa uchunguzi ulikuwa unafanywa kuhusu madai ya kampuni ambayo mke wa Mchechu ni mkurugenzi kupewa mkataba wa kutoa bima kwa ajili ya nyumba za shirika mkoani Mtwara jambo ambalo ni kinyume cha kanuni za utumishi wa umma juu ya mgongano wa kimaslahi.

Kadhalika, kwa mujibu wa habari hiyo, vyanzo vya habari vilibainisha kwamba kamati iliyoundwa kuchunguza matumizi mabaya ya ofisi ndani ya NHC ulionyesha ukiukwaji mkubwa na matumizi mabaya ya kutisha ya fedha za umma uliofanywa na Mchechu.

**USHAHIDI WA MCHECHU**

Katika ushahidi wake mahakamani juu ya habari hiyo, Mchechu alidai kwamba haina hata chembe ya ukweli isipokuwa ililenga kumchafua na kumharibia heshima yake aliyoijenga katika jamii kwa muda mrefu.

Alidai kuwa kulingana na madai ya habari hiyo, NHC haijawahi kununua ekari 500 jijini Arusha kwa ajili ya mradi wa Safari City bali ekari halisi ni 583 na kwamba hajawahi kuchunguzwa kutokana na bodi ya shirika au taasisi yoyote ya uchunguzi ikiwamo TAKUKURU kuhusu mradi huo na kwamba hana ardhi karibu na mradi huo kama ilivyodaiwa.

Mchechu alidai kwamba ardhi anayodaiwa kuiuzia NHC si kweli kwa kuwa hajawahi kumiliki ardhi katika mkoa wa Arusha katika maisha yake wala hana kampuni iliyowahi kufanya hivyo. Pia alidai hajawahi kuiuzia NHC ardhi popote Tanzania.

Pia alidai kwamba hawajahi kuingilia masuala ya ununuzi akiwa mtendaji mkuu wa shirika na hajawahhi kupoka mamlaka hayo. Kuhusu madai ya kampuni ya mke wake, alidai kwamba halijawahi kufanyika jambo kama hilo na kwamba NHC haikati bima kwa ajili ya mali zake zikiwamo nyumba.

Kuhusu uchunguzi wa matumizi mabaya ya ofisi na matumizi mabaya ya fedha za umma, bosi huyo wa NHC alidai kuwa hakuna kitu kama hicho na hakujawahi kuwapo taarifa ya uchunguzi iliyomtia hatiani kwa matumizi mabaya ya fedha za umma na ukosefu wa maadili.

**ATHARI**

Kutokana na habari hiyo, Mchechu alisema licha ya kumshushia hadhi, alikosa kuaminika, hivyo kupoteza nafasi nyingi za kibiashara alizokuwa anafanya pamoja na kuondokewa na wabia katika kampuni ambazo ana uhusiano nazo kibiashara.

"Taarifa hii ilinisababishia mfadhaiko mkubwa wa akili, msongo wa mawazo hofu na kudhuru afya yangu. Pia ilinipotezea nafasi ya maendeleo yangu kikazi na kunipotezea mapato ya ajira yangu na ushiriki wangu katika bodi mbalimbali ndani na nje ya nchi," alidai huku akiongeza kuwa alilazimika kujiuzulu baadhi ya nyadhifa.

Mchechu pia alidai mahakamani kwamba wakati habari hiyo inaandikwa alikuwa katika mchakato wa kupata nafasi ya ofisa mtendaji mkuu wa taasisi ya kimataifa ya kifedha ya Shelter Afrique, hivyo kusababisha kukosa licha ya kwamba alikuwa akiongoza katika mchakato huo.

Pia kutokana na nafasi yake ya uongozi katika kanisa, akiwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Fedha ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, alikosa kuaminika na kuwapo hofu ya usalama wa sadaka za waumini.

"Kwa kweli habari hii imenifanya nionekane mlafi, tapeli, mlanguzi, mtu anayetumia vibaya nafasi yake. Pamoja na mambo mengine, naiomba mahakama nisafishwe na chombo hiki na nilipwe fidia kutokana na athari na hasara nilizopata," alidai.

# Wadau, watumishi wafurahia kupanda viwango mishahara

**Na Waandishi Wetu**

WADAU na watumishi wa serikali wamepongeza uamuzi wa serikali wa kupandisha mishahara huku wakisema Rais Samia Suluhu Hassan, ametekeleza ahadi yake siku ya Mei Mosi, mwaka huu kwa vitendo.

Juzi, Rais Samia, aliridhia mapendekezo ya kuongeza mishahara ikiwamo kima cha chini kwa watumishi wa umma kuwa kwa asilimia 23.3, huku ikielezwa Sh. trilioni 1.59 zitatumika katika ongezeko hilo.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, ilisema serikali imepanga kutumia Sh. trilioni 9.7 katika mwaka wa fedha 2022/23 kwa ajili ya kugharamia malipo ya mishahara ya watumishi wote katika serikali kuu, serikali za mitaa, taasisi na wakala za serikali.

Katibu wa Halmashauri Kuu Taifa, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema uamuzi huo ni mwendelezo wa hatua kadhaa zinazoendelea kuchukuliwa na serikali ya CCM awamu ya sita.

"Tayari serikali ilishapunguza kodi ya mapato katika mishahara ya wafanyakazi (PAYE) kutoka asilimia tisa hadi nane, kufuta tozo ya kulinda thamani ya mkopo ya asilimia sita (Value Retention Fee) kwa wanufaika wa mikopo elimu ya juu wakati wa marejesho na upandishwaji wa madaraja kwa kuzingatia miundo ya utumishi wa kada mbalimbali," alisema Shaka.

Aliongeza kuwa hatua zote hizo ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 -2025, ibara ya 130, ukurasa wa 180-181.

Naye Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Njombe, Scolastika Kevela, alipongeza na kusema imeonyesha jinsi Rais Samia alivyo mlezi mzuri kwa wafanyakazi wake.

Hapiness John mkazi wa Mbezi Makabe, alisema uamuzi wa Rais kuridhia nyongeza ya mshahara umekuja wakati mwafaka kutokana na vitu kupanda bei mfululizo hivyo itasaidia kupunguza gharama za maisha.

"Rais amekuwa kama mkombozi katika kipindi hichi, hicho alichokiongeza sio kwamba kitamaliza shida zetu, ila kitapunguza mzigo wa maisha kwa kiasi fulani, maana sasa hivi kila kitu kimepanda kuanzia vyakula hadi huduma za usafiri," alisema.

Alisema kitendo hicho pia kitawaheshimisha watumishi kwa kuwa hapo zamani kazi ya utumishi, ilikuwa ikikimbiwa kutokana na mishahara kuwa midogo.

"Zamani utumishi ilikuwa inaonekana kama kujitolea, watu walikuwa wakikimbili sekta binafsi kwa sababu ya unafuu wa mishahara, lakini sasa Rais anaweka usawa katika ya sekta hizi mbili, ni jambo la kumshukuru," alisema.

Rais alitoa ahadi ya nyongeza ya mshahara kwa watumishi katika sherehe za Siku ya Wafanyakazi (Mei Mosi) mwaka huu, ingawa si kwa kiwango walichokipendekeza

Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA) cha Sh. milioni 1.01 kwa mwezi kwa sababu ya hali ya uchumi wa taifa na dunia siyo nzuri.

Juzi, Rais wa TUCTA, Tumaini Nyamhokya, alinukuliwa na vyombo vya habari (si Nipashe) akimshukuru Rais Samia kwa kuwajali watumishi wa umma, kwa kuwa nyongeza hiyo italeta ahueni kubwa.

"Suala la nyongeza ya mishahara tumelipokea vizuri kwa sababu ni ahadi yake ya Mei Mosi aliposema tuna jambo letu na tumpe muda wakaone watapandisha kiasi gani. Tunamshukuru kwa kutujali wafanyakazi, mwaka jana alipandisha madaraja na wengine mpaka leo wanaendelea kupanda madaraja," alifafanua.

**Imeandikwa: Jenifer Gilla na Beatrice Shayo**

HABARI KITAIFA

# Kibano chaja halmashauri mapato kiduchu

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, inakusudia kuzichukulia hatua kali halmashauri na mikoa itakayoshindwa kufikia asilimia 80 ya makusanyo ya mapato ya ndani ifikapo mwishoni mwa mwaka huu wa fedha.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Abdallah Chaurembo, alisema juzi mkoani hapa wakati wa akipokea taarifa ya makusanyo ya mkoa kwenye ziara ya kamati hiyo ambayo iliyotembelea miradi mbalimbali inayotekelezwa na serikali kupitia Mpango wa Kurasimisha Rasilimali za Biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA).

Chaurembo alizitaka halmashauri kuongeza juhudi mbalimbali zitakazowezesha usimamizi wa makusanyo ya fedha kwa kipindi cha mwezi mmoja, ili zitumike kwa maendeleo ya uchumi na huduma za kijamii.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, alisema mbali na MKURABITA kuanzishwa kwa lengo la kuwapa nguvu ya kiuchumi wananchi kwa kuwaongezea uwezo wa kumiliki na kufanya biashara katika mfumo unaozingatia utawala na sheria, imekuwa ikifanya na taasisi mbalimbali za kifedha hapa nchini.

Alisema MKURABITA inafanya kazi licha ya kazi zake baadhi kutoonekana wazi, akieleza namna mkoa wa Dodoma waendesha usafiri wa pipikipi walivyonufaika kupitia moja ya kufanyika mpango mkakati wa kuliwezesha kiuchumi kundi hilo.

Mtendaji Mkuu MKURABITA, Dk. Seraphia Mgembe, alisema mpango umetekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo mbalimbali nchini ikiwamo Morogoro kwa kushirikiana na halmashauri za manispaa na wilaya ikiwamo utoaji mafunzo kwa wananchi, umiliki wa biashara na kuendeleza miradi hiyo.

Pia alisema mpango huo umefanikiwa kutoa wazo la namna ya kukuza huduma ya usajili na utoaji wa leseni za biashara kwa halmashauri la kujengwa kwa vituo vya utoaji huduma za pamoja (One Stop Centre).

Naye Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, alisema katika utekelezaji wa makusanyo mkoa huo una deni la asilimia 17, ili kufika asilimia 100 na kwamba wameweka mkakati wa kusimamia watendaji waliopewa jukumu la ukusanyaji ndani ya muda uliobaki.

# Royal Tour yasukuma kufumuliwa sera, sheria

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema itafanya mabadiliko ya sheria na sera, ili kukidhi mabadiliko yatakayotokana na Royal Tour kwa kuwa sekta ya utalii haikupewa kipaumbele wakati wa kutungwa kwake.

Akizungumza mwishoni mwa wiki wakati wa kikao cha mtandaoni kuzungumzia mafanikio ya filamu hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Prof. Godius Kahyarara, alisema kuna fursa kubwa ya kuongeza uwekezaji nchini na kwamba walifanya kikao na wadau wa sekta binafsi na kubaini kuna umuhimu wa kubadilisha sera na sheria ili kukidhi mahitaji na mabadiliko.

"Kwenye uwekezaji tuko kwenye hatua za mwisho za kubadili sheria ya mwaka 1997 ambayo imepitwa na wakati, imeanzishwa kabla hatujaingia kwenye East African Common Market, vitu vingi vimebadilika lakini sheria imebaki nyuma," alisema.

Kwa mujibu wa Prof. Kahyarara, ni muhimu kuwa na sheria inayoangalia uhalisia kwa kuangalia vitu vinavyohitajika sasa na kwa namna gani inatoa nafasi kwa uwekezaji ikiwamo vivutio, na kwamba watazingatia kwenye mabadiliko ya sheria.

"Tunatarajia kufanya mabadiliko ya sera ya uwekezaji ya mwaka 1996 iliyoangalia uchumi wa Tanzania kwa miaka ya nyuma sana, na kwamba mabadiliko mengi yaliyokea miaka ya 90, kama tuna sera mwaka 96 haiko mbali na tulikotoka miaka ya 60, kwasasa tumeshuhudia mambo mengi yamebadilika sana.

"Sekta ya utalii haikuwa kipaumbele, wakati huo ilikuwa ni kilimo ndiyo kinaajiri, ndiyo maana tunasema lazima sera na sheria iangalie masuala ya utalii na mengine ambayo ni kipaumbele kwa sasa," alisema.

Alisema kuna sekta nyingine ambazo wamekubaliana kuziangalia sheria na sera zinazohitaji kubadilishwa ili kuendana na mabadiliko yatakayoletwa na Royal Tour, na kwamba uchumi wa nchi utabadilika na kwamba ni ubunifu mkubwa.

Prof. Kahyarara alisema uwekezaji umeongezeka kwa asilimia 800, na kwamba Royal Tour ni kichocheo cha watu kuwekeza kwenye biashara na utalii, na kwamba kati ya mikataba saba iliyoingiwa Marekani mmoja ni wa kuimarisha utalii ambao ni wa kampuni kubwa.

"Jana tumefuatilia tumeona watu wengi wanaulizia sekta ya utalii, tunaona ubunifu na kuna vitu vingi vinaweza kufanyika kwenye uwekezaji, kuna watu wako tayari kuingia kwenye sekta hiyo na wengine wamejisajili na Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kwa kuwa wanaona kuna sababu ya kuwekeza fedha zao," alisema.

Naye Katibu Mkuu wa Wizara ya Utalii na Mambo Kale, Zanzibar, Fatuma Mabrouk Khamis, alisema filamu hiyo itaongeza wageni kwa kuwa imetengeneza sababu ya watu kuja kutumia fedha zao, ambazo zitakuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Mwenyekiti wa Kamati ya Royal Tour, Dk. Hassan Abbas, alisema hadi sasa Royal Tour alisema "Kupitia filamu hii Rais amefanya mahojiano maalum na vyombo vingi duniani, na ataendelea kufanya hivyo ikiwa ni mkakati wa kuitangaza Tanzania duniani. Habari zake (Rais) zimechapishwa kwenye magazeti zaidi ya 30 duniani, hadi jana (juzi) taarifa za filamu yetu zimewafikia watu milioni 546, ni sehemu ya mkataba ule ule wa filamu yetu."

Alisema takwimu hizo zinaonyesha kuwa watu 530 walisoma na kusambaza taarifa hizo kwa watu wengine kwa kuzipeleka mbali zaidi, pia alikutana na wadau watano ikiwamo mwekezaji namba moja wa hoteli duniani, mmiliki mtandao wa mawakala wa utalii duniani, anayemiliki meli za kifahari, majumba mengi duniani ya kuonyesha 'theater', na kwamba manufaa ni makubwa zaidi ya filamu yenyewe.


## JOB VACANCIES ANNOUNCEMENT

### PHARMACEUTICALS AND MEDICAL DEVICES SALES REPRESENTATIVE

We are a Pharmaceutical, and Medical Devices Company. We import and distribute Pharmaceuticals and Medical Devices from Europe, Asia and other parts of the global.

We are looking for the qualified, motivated, people-oriented candidates to fill the job vacancies listed below in our company. The Pharmaceuticals and Medical Devices Sales Representative will be responsible for sales, promotion and marketing of our products. We also looking for a Biomedical Technician who will do the Repairs, services and installations of Medical Equipment.

**Job Title**

**1. Pharmaceutical Sales Representatives**

| Work Place | Number of Post |
|---|---|
| Arusha | 2 Posts |
| Dodoma | 2 Posts |
| Mwanza | 2Posts |
| Morogoro | 1post |
| Mbeya | 2 Posts |
| Zanzibar | 1 Post |
| Moshi | 1 Post |
| Dar es Salaam | 5 Post |

**2. Medical Devices Sales Representatives**

| Work Place | Number of Post |
|---|---|
| Dar es Salaam | 1 post |

**3. Biomedical Technician/Engineer**

| Work Place | Number of Post |
|---|---|
| Dar es Salaam | 1 Post |

**Key Requirement and Qualifications**

1. Diploma or Degree in the relevant field
2. Relevant Job Experience of more than two years.
3. The applicants must be willing to travel with little notice and havea good working knowledge of Tanzania regions.
4. Applicant should have good English and Kiswahili communication skills that will enable them to:

(i) Work on development and implementation of key marketing programs.
(ii) Provide Market updates, expense reporting and other required business reporting
(iii) Develop customer relationships and maintain a high level of customer satisfaction.
(iv) Proactively prospect for new customers and new opportunities.
(v) Solve a broad range of problems of varying scope and complexity.
(vi) Provide prompt response to all customer requests.
(vii) Applicant should have record of accomplishment of achieving sales targets around quota and sales forecastsand proactively drive the salescycle and forecastsales.
(viii) Applicant should have excellent computer skills to be able to make reports and presentations.
(ix) Applicant should be able to demonstrate

**Core Values of:** Innovation, Trust, Respect, Teamwork, Uncompromising Integrity, Speed, Focus and Accountability

**Mode of Application:**

**To apply, kindly submit your application with a detailed CV, photocopies of academic and other relevant certificates and names of three referees with their contacts to The Advertiser, P.O BOX 40385, DAR ES SALAAM, within two weeks form the date of this advertisement.**

**Please indicate your preferred work Station**

**Only short listed candidates with proven requirements and experience will be contacted.**

MAKALA MAALUM

# Royal Tour na fursa lukuki uwekezaji mkoani Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA



Rais Samia

KUANDALIWA kwa filamu ya Tanzania The Royal Tour kumelenga kutangaza vivutio vya utalii vilivyoko nchini. Mbali na madhumuni hayo, filamu hiyo pia ni miongoni mwa fursa muhimu za Tanzania kujitangaza na kujiimarisha kiuchumi kupitia maeneo mbalimbali.

Pamoja na kwamba filamu hiyo imebeba maudhui ya utalii, ni njia moja wapo ya kuonyesha namna Tanzania ilivyobarikiwa kwa kuwa rasilimali ambazo zikitumika ipasavyo, zitavuta watalii na wawekezaji wengi kuwekeza nchini.

Tayari filamu hiyo imeshazinduliwa katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, visiwani Zanzibar na jana ilikuwa ni zamu ya Mkoa wa Dodoma ambao umeizindua kwa kunadi fursa lukuki zilizoko maeneo mbalimbali mkoani hapa.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, akizungumzia uzinduzi wa filamu hiyo, anasema wameamua kufanya uzinduzi wa aina yake unaotangaza fursa zilizoko na wafanyabiashara kutoa ushuhuda namna Royal Tour itakavyosaidia kuwafungulia fursa zaidi za kujikwamua kiuchumi.

Mtaka anasema Dodoma ni eneo linalofaa kwa uwekezaji na ujenzi wa viwanda vikubwa kutokana na kuwapo kwa ardhi kubwa.

"Kwa Dodoma uzinduzi huu ni wa tofauti kwa sababu tunataka sekta binafsi izungumze manufaa na fursa za filamu hii zitakavyofungua milango ya uwekezaji na ufanyaji biashara.

"Dodoma ni Makao Makuu ya Nchi, tuna fursa ya utalii wa utamaduni wa makabila ya hapa, utalii wa miradi, utalii wa zabibu, utalii wa maliasili, kuna fursa ya kuwekeza viwanda lakini kujenga nyumba za kupangisha au kuuza.

"Hawa wageni watakaovutiwa na Tanzania, wengine wanaweza kutamani kumiliki nyumba Dodoma, tuna fursa nyingi zinahitaji uwekezaji ili Dodoma ifunguke kiuchumi na wananchi wetu vipato vyao vipae," anasema.

Anatoa wito kwa Watanzania na wakazi wa Dodoma kuchangamkia fursa hiyo muhimu ambayo Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha njia na itakuwa na matunda kwa Taifa.

**FURSA ZA KILIMO DODOMA**

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatma Mganga, anasema mkoa huo una fursa nyingi za kilimo na ufugaji nyuki na kutoa wito kwa wawekezaji kuchangamkia fursa hizo kwa kuwa tayari kuna mashamba makubwa ambayo yamepimwa, yana hati na yanafaa kuwekeza kwenye kilimo cha alizeti, mtama na zabibu.

"Kuna mashamba yapo Wilaya za Chamwino na Bahi, kilimo ni kitu kinachoweza kuleta fedha nyingi sana. Kwa mfano, Afrika Kusini unakuta mtu ana shamba kubwa, yaani kulitembelea ni kama unafanya safari ndiyo tuna fursa za mashamba ya aina hii Dodoma ambayo yanahitaji uwekezaji," anasema.

Katibu Tawala huyo pia anasema zabibu ya Dodoma ni zao la kipekee kutokana na kuvunwa mara mbili kwa mwaka na kwamba hiyo ni fursa inayohitaji uwekezaji kwa wageni watakaochangamkia fursa za Tanzania The Royal Tour.

"Kwenye alizeti sisi ni miongoni mwa mikoa minne ya kimkakati ya kilimo cha alizeti, tunahitaji uwekezaji kuwa na mashamba makubwa ya kilimo hiki ambacho kina soko, kama mnavyojua mahitaji ya mafuta ya kula kwa mwaka ni makubwa na uzalishaji ulipo sasa haukidhi mahitaji, lakini ardhi yetu tuliyo nayo inafaa kwa kilimo hiki," anasema.

Akizungumzia zao la mtama, Katibu Tawala huyo anasema ni zao ambalo kwa sasa lina soko na linahitaji wananchi na wawekezaji kulima kwa wingi kutokana na kupatikana kwa soko katika Shirika la Chakula Duniani (WFP).

Mchumi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Francis Kaunda, anasema kuna mashamba makubwa 171 eneo la Zuzu ambayo yamewekewa miundombinu yote ikiwamo bwawa lisilokauka kwa ajili ya umwagiliaji.

"Hili eneo tunaita 'urban farming', kuna miundombinu yote muhimu na lipo katika barabara ya mzunguko (ring road) inayojengwa, ukubwa wa mashamba unaanzia mita za mraba 4,047 (ekari moja), mashamba haya yanahitaji watu waje kuwekeza na kila mita ya mraba inauzwa Sh. 3,000 na yanafaa kwa kilimo cha mboga, alizeti na zabibu," anafafanua.

Anasema pia kuna fursa ya uwekezaji wa mashamba ya kufuga wanyamapori ambayo itawawezesha watu kutengeneza mbuga ya wanyama na kuongeza vivutio vya utalii ndani ya jiji hilo.

**ENEO LA KUJENGA VIWANDA**

Mchumi huyo anasema Jiji la Dodoma pia limetenga eneo Nala jijini hapa lenye ukubwa wa ekari 2,094 ambalo lina uwezo wa kuchukua viwanda vikubwa zaidi ya 100.

Anasema eneo hilo lina miundombinu yote huku akitolea mfano kiwanda cha mbolea asilia cha Itracom ambacho ujenzi wake upo kwa asilimia 80, kwamba kwa sasa kuwa ni miongoni mwa viwanda vikubwa vinavyofaa kujengwa kwenye eneo hilo.

"Tuna eneo la Mpunguzi wawekezaji wataweza kulima zao la zabibu na kuanzisha viwanda vingi vya wakulima wadogo wa zabibu," mchumi huyo anafafanua.

Kuhusu usalama, mchumi huyo anasema jiji lina mpango wa kuimarisha usalama kwa kufunga kamera kwenye mitaa ili kuimarisha usalama wa wananchi na mali zao na kuvuta wawekezaji.

"Pamoja na kuita wawekezaji, hatujawasahau wafanyabiashara wetu wadogo, tunajua Royal Tour italeta wageni na watakuwa na mahitaji yao mbalimbali. Tumejenga soko la kisasa la Machinga, limegharimu Sh. bilioni 7.5, hili ni soko la kipekee, lina huduma zote pale na limejengwa kwa kushirikisha wanufaika, litakuwa na uwezo wa kuchukua wafanyabiashara wadogo zaidi ya 3,000," anasema.

**WAFANYABIASHARA WAFUNGUKA**

Rais wa Sauti ya Wanawake Wajasiriamali Tanzania, Maida Waziri, anasema filamu hiyo ambayo imechezwa na Rais Samia Suluhu Hassan, italitangaza Taifa na wafanyabiashara watanufaika kwa kiasi kikubwa na fursa hizo.

"Kuna manufaa makubwa ya Royal Tour yanakuja kwa private sector (sekta binafsi), kuna watu wamekuwa wakibeza juhudi hizi za Rais Samia lakini sisi taasisi binafsi tumeanza kuona manufaa makubwa sana katika nyanja zote," anasema.

Mfanyabiashara huyo anasema miongoni mwa manufaa ni miradi katika sekta za ujenzi na kilimo pamoja na kuongezeka ajira na watalii.



Mratibu wa kikundi cha WhatsApp Together we Fight, Gwakisa Mwasyeba (kushoto), akikabidhi msaada wa vitu mbalimbali kikiwamo chakula kwa niaba ya wanakikundi wapatao 150 katika kituo ambacho kinatoa elimu kwa watoto wenye matatizo ya utindio wa ubongo cha Brothers of Charity kilichoko Kitangili Manispaa ya Shinyanga, juzi, (kulia) ni mkuu wa kituo hicho George Rice. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Pinda asisitiza misingi uongozi bora

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amesema falsafa ya misingi bora ya uongozi iliyowekwa na Hayati Mwalimu Julius Nyerere inapaswa kurithishwa kwa vijana nchini ili kuendelea kuenzi tunu hiyo.

Pinda alisema hayo mwishoni mwa wiki kwenye Kongamano la Miaka 100 ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Uzinduzi wa Kitaifa wa Taasisi ya Kumbukumbu ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere yenye kaulimbiu, "Kujitawala ni Kujitegemea."

Alisema falsafa hizo zilizowekwa na Mwalimu Nyerere wakati wa uhai wake bado zinaendelea kuishi licha ya yeye kufariki dunia.

Pinda ambaye alimwakilisha Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kwenye uzinduzi huo, alisema kuanzishwa kwa taasisi hiyo ni kwa ajili ya kuwasaidia vijana wajue na kuyaenzi mazuri ya Mwalimu na kwamba alikuwa kiongozi si wa Tanzania bali ulimwengu mzima.

"Katika kuenzi mazuri ya Mwalimu ambaye alijali utu wa watu, alijishusha na kuenzi utamaduni wa kujisahihisha nataka Wizara za Elimu, Wizara ya Utamaduni, Wizara ya Habari, Wizara ya Mambo ya Nje, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na taasisi binafsi kuenzi tunu hizi za mwalimu kwa kukusanya, kuhifadhi na kutambua nyaraka na kumbukumbu kwa ajili ya vizazi vijavyo," aliagiza.

Pinda ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Taasisi hiyo, alipongeza Mpango wa miaka 10 wa Wizara ya Maliasili na Utalii wa kukusanya, kuhifadhi na kutangaza tunu za Mwalimu Nyerere na kutaka wahakikishe wanatekeleza programu ya kutunza na kuhifadhi malikale zote zinazohusu Mwalimu Nyerere.

Naye Mwenyekiti wa Kitaifa wa Taasisi hiyo, Paul Kimiti, alisema Watanzania wanatakiwa kuyaenzi mazuri yaliyoanzishwa na Mwalimu Nyerere kama amani, utulivu na mshikamano kwa kuendelea kushikamana.

Naibu Waziri wa Maliasili, Mary Masanja, alisema wizara imejipanga kukusanya na kutunza kumbukumbu za viongozi waasisi nchini.

Awali, akitoa mada ya uendelezaji na uimarishaji wa misingi ya amani na mshikamano wa kitaifa, Prof. Palamagamba Kabudi, alisema dunia inatekeleza falsafa, misingi na sera kupitia Mpango wa Maendeleo Endelevu na Mipango wa Millenia ambayo Mwalimu Nyerere aliiandaa.

Naye Makamu Mwenyekiti mstaafu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Philip Mangula, alisema vijana wanatakiwa kuendelea kuenzi elimu ambayo Mwalimu alisimamia kwa kuwa ni silaha bora katika kupambana na umaskini, ujinga na maradhi.

# Mganga kienyeji mbaroni madai kulawiti watoto

**Na Neema Hussein,** MPANDA

JESHI la Polisi mkoani Katavi, linamshikilia mganga wa kienyeji, Akili Abakuki, maarufu Jimmy (38), mkazi wa Majengo, Manispaa ya Mpanda kwa tuhuma za kuwalawiti watoto sita nyakati za usiku alipokuwa akiwapatia matibabu ya tiba za asili.

Kaimu Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Katavi, Sylvester Ibrahim, alisema juzi mtuhumiwa huyo alikamatwa Mei 8, majira ya saa 7:00 mchana katika eneo la Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Katavi, mjini hapa.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa baada ya mama mmoja kugundua mtoto wake wa miaka 10, mwanafunzi wa darasa la tatu (jina limehifadhiwa) aliyekuwa amempeleka kwa mganga huyo kupatiwa matibabu ya asili, amelawatiwa.

Kamanda wa Ibrahim alisema baada ya kupatikana taarifa hizo, Jeshi la Polisi lilifanikiwa kumkamata mtuhumiwa huyo ambaye alikuwa amewalawiti watoto wengine watano wakati akiwafanyia matibabu. Watoto hao wanao mri kati ya miaka sita na 12.

Alisema wazazi wa watoto hao walikuwa wakiwapeleka kwa mganga huyo kwa ajili ya kupatiwa tiba za asili na katika tiba hizo, mganga huyo alikuwa akitoa masharti lazima azitoe usiku, hivyo ni lazima watoto hao walale kwake bila wazazi wao kuwapo.

"Ilipokuwa ikifika usiku, mganga huyo alikuwa anawadanganya kwa kuwapatia zawadi ndogo ndogo kama pipi, biskuti na jojo na kisha anawavua nguo na kuwapaka mafuta mwili mzima na kuwalawiti.

Kamanda Ibrahim alisema vitendo hivyo vya kuwalawiti watoto hao alikuwa akivifanya ndani ya chumba chake alichokuwa akiishi usiku wa manane huku akiwatishia atawafanyia kitu kibaya iwapo watawaambia wazazi wao kuwa amewafanyia kitendo hicho.

Kutokana na kuwapo kwa hali hiyo, kamanda amewahimiza wazazi mkoani Katavi kufuatilia vitendo ambavyo wanaweza kuwa wamefanyiwa watoto wao na pia wazazi waache tabia ya kuamini imani potofu za kishirikina.


**NYUMBA YA MAKAZI INAUZWA**

IKO MAKONGO JUU UPANDE WA DTV, KARIBU NA HOSTEL MPYA ZA CHUO CHA ARDHI

NYUMBA YA MATOFALI INA VYUMBA TISA NA ENEO LA KUEGESHA MAGARI MATATU NA HATI KAMILI

116856902

**MAWASILIANO**

**0719 - 060817 - TWALIB H. MOHAW**

**0744 - 227395 - ADIJA T. MOHAW**



**UDHAMINI WA MAFUNZO YA UFUNDI**

**KCB Bank Tanzania** kupitia **KCB Foundation** kushirikiana na Shirika la Kijerumani **Deutcsche Gessellschaft Internationale Zusannebarbeit (GIZ)** na **programu ya Ajira na Ujuzi kwa Maendeleo Afrika (E4D)** inatoa udhamini wa masomo kwa vijana wa umri kati ya miaka 18- 35 katika fani ya ujenzi kupitia kozi fupi.

Mnufaika wa udhamini huu atapata mafunzo ya ufundi ya darasani, atajifunza ufundi kwa vitendo, ujuzi wa maisha kiujumla, namna ya kupata ajira na kujiajiri kupitia fani ya ujenzi.

Mradi huu ni wa kipindi cha 2021-2023, na mikoa itakayonufaika ni Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro, Arusha, Moshi bila kusahau Zanzibar.

Ufadhili huu unatolewa kupitia Taasisi ya VETA ama taasisi nyingine yoyote ya serikali ya maeneo tajwa kwa kipindi cha miezi 3 hadi 6. Mwombaji atatunukiwa cheti pindi amalizapo mafunzo haya kwa ufaulu.

Kwa mawasiliano zaidi, tupigie kupitia namba hizi hapa: **0737 883 708/ 0715 656 599 / 0743 400 089**

KCB FOUNDATION

Implemented by giz Norad E4D 2JiA JiRi

**VIGEZO NA MASHARTI**

- Ni kwa vijana wenye umri kati ya miaka 18-35
- Wanaojua kusoma na kuandika
- Wenye kitambulisho cha Taifa/Mpiga kura/ Leseni ya Udereva/ barua ya utambulisho kutoka Serikali ya mtaa wako
- Wenye utayari kusoma kozi za ufundi stadi



Wanufaika wakiwa na barua za kuchaguliwa rasmi kuanza masomo katika fani ya Ujenzi.



Hivi ndivyo usahili ulivyofanyika jijini Morogoro.



Mmoja wa wanufaika akikabidhiwa barua ya kujiunga rasmi katika udhamini wa masomo




Mnufaika wa Udhamini akiwa ameshikilia vifaa vyake vya kujilinda atakavyovitumia wakati wa masomo yake ya ujenzi

216855402

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Waamuzi wapongezwe kama wanavyolaumiwa

**LIGI** Kuu Tanzania Bara sasa imeingia raundi ya 24 kwa michezo minne kuchezwa mwishoni mwa wiki ambapo Mbeya City ilikuwa nyumbani ikiikaribisha Polisi Tanzania huku Mtibwa Sugar ikiwa mwenyeji wa Coastal Union na Dodoma Jiji FC ikiwaalika vinara wa ligi hiyo, Yanga.

Raundi hiyo ya 24 itakamilika wiki hii, hiyo ikimaanisha sasa zitakuwa zimebaki mechi sita kwa kila timu kabla ya ligi hiyo kumalizika na bingwa wa msimu huu wa 2021/22 kujulikana rasmi.

Hadi Ligi Kuu inaingia raundi hii ya 24, bado Yanga ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 57, ikifuatiwa na bingwa mtetezi, Simba aliyepo nafasi ya pili kwa tofauti ya pointi nane kabla ya mechi za jana.

Hata hivyo, vita kubwa katika ligi hiyo imekuwa kuanzia nafasi ya tatu hadi ya 11, kwani timu hizo zinapishana alama moja hadi nne huku zinazofuata hadi mkiani zikipishana pointi moja hadi tano, hivyo hata inayoshika nafasi ya tatu inaweza kushuka daraja isipochanga karata zake vema.

Mbali na vita hivyo vya kuepuka kushuka daraja, pia vinasindikizwa na vile vya kuwania kumaliza nafasi nne za juu, ili kupata nafasi ya kushiriki michuano ya kimataifa msimu ujao.

Vita hivyo, haviishii hapo tu, bali pia nyuma yake kuna kuwania kumaliza nafasi ya juu ili mwisho wa msimu kuibuka na bonasi nzito itakayotolewa na wadhamini wa haki za matangazo, Kampuni ya Azam Media Limited.

Hiyo ni kutokana vipengele katika mkataba huo wa miaka 10 walioingia na TFF, kuahidi kutoa bonasi ya Sh. milioni 500 kwa bingwa, nafasi ya pili Sh. milioni 250, ya tatu milioni 225/-, ya nne milioni 200/- ya tano milioni 65 na zitakwenda zikipungua hadi timu itakayoburuza mkia ikipata kifuta machozi.

Lakini pamoja na Yanga kuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, bado inapaswa kuendelea kushinda ili kuweza kujihakikishia ubingwa huo baada ya kuambulia sare tatu mfululizo kabla ya mchezo wao wa jana, ugenini dhidi ya Dodoma Jiji FC.

Kutokana na sababu hizo, kuna kila sababu kwa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Bodi ya Ligi (TPLB) na Chama cha Waamuzi (FRAT) chini ya kamati zake, kwa pamoja kuongeza umakini kwa waamuzi ili kuchezesha kwa haki, na haki ionekane ikitendeka kweli.

Tunataka kuona kila timu mwisho mwa msimu ikimaliza nafasi iliyostahili na si kwa ajili ya kubebwa kwa namna yoyote ile kwani kwa kufanya hivyo kutasababisha kupata wawakilishi wabovu kwenye michuano ya kimataifa msimu ujao na hilo litaepukika tu kama waamuzi watatenda haki.


Hata hivyo, hadi kufikia raundi hii ya 24, hatuna budi kuwapongeza waamuzi husuan katika mzunguko wa pili, kwani wamepunguza makosa mengi ambayo yalikithiri kwenye duru la kwanza.

Lawama nyingi ambazo zilikuwa zikielekezwa kwao zimepungua, ingawa makosa hayajaisha kabisa lakini yamepungua kwa kiasi kikubwa na ndiyo maana kwa kipindi kirefu sasa walioadhibiwa kwa kushindwa kumudu ama kutafsiri sheria za soka wakipungua.

Kutokana na hilo, Nipashe tunaona ipo haja ya kutoa kongole kwao zikienda sambamba na kadri walivyokuwa wakilaumiwa na si kusubiri hadi makosa yanapokithiri kutoka kwao tuanze kuwashushia lawama.

Wakifanya vizuri tuwapongeze ili wanapovurunda tuwalaumu pia. Lakini pamoja na pongezi hizo kwa waamuzi, tunachotaka kuona kwao ni kuongeza umakini kwa kufanya vizuri zaidi na si kuanza kubweteka na kujikuta wakiishi kwa kuangukia katika methali ya "Mgema akisifiwa, tembo hulitia maji".

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kuna tatizo pasi za mwisho wachezaji soka la Bongo

Na Adam Fungamwango

**IMEKUWA** ikielezwa kuwa nchini Tanzania kuna tatizo la mastraika na mabeki wa kati, lakini hakuna sana uhaba wa mabeki wa pembeni pamoja na viungo washambuliaji.

Inaonekana kwa jicho la kawaida ni kweli, lakini kama tunakwenda kwenye takwimu inabidi tuangalie upya, kwani inawezekana tukawa na mabeki wa pembeni machachari, lakini si hatari.

Inawezekana pia tukawa na viungo washambuliaji wenye uwezo mkubwa wa kupiga chenga, kanzu, na kucheza soka la kufurahisha mashabiki jukwaani na si kuisaidia timu.

Nimeandika hili kutokana na kushangazwa na pasi za mwisho kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa. Inasikitisha, kuhuzunisha, kushangaza na kuchekesha kwa wakati mmoja kuwa eti mpaka sasa wakati ligi ipo ukingoni kabisa wanaoongoza kwa kupiga pasi za mwisho wana 'assist' nne tu.

Kwa ligi hii ambayo ina timu 16 na kila timu inatakiwa kucheza mechi 30, huku tukiwa katika raundi ya 23, wanaoongoza kwa 'assist' wawe nazo nne tu.

Kifupi tu kwamba hapa kuna tatizo. Angalau tungeweza kumpata mwenye 'assist' saba mpaka nane hadi kufikia hatua hii na hata kama asipotoa tena hadi ligi inamalizika, si mbaya, lakini nne kwa raundi ya 23 ni ndogo sana.

Kwenye mchezo wa mpira wa miguu 'assist' hutolewa na mchezaji yeyote yule hata kipa. Lakini mfumo wa soka mara nyingi pasi za mwisho hutolewa na wachezaji wanaocheza nafasi ya viungo washambuliaji, kama vile namba nane na kumi.

Pia kwa mfumo wa soka la kisasa, mabeki wa pembeni ambao kazi yao mama ni kuzuia mashambulizi, lakini nao hupanda mbele kwenda kuongeza mashambulizi, hivyo kazi namba mbili ni kupiga krosi, au kutoa pasi ambazo zote hizo ni 'asssist' kwa ajili ya mastraika au wachezaji wengine kupachika mabao.

Nimeona wachezaji vinara wa pasi za mwisho, eti hata mastraika nao wanaongoza kwa kutoa 'assist' badala ya viungo. Reliants Lusajo wa Namungo, na Pius Buswita wa Ruvu Shooting.

Kwa idadi ya 'assist' zao ni sawa kwa sababu wao ni mastraika, lakini kuongoza inanifikirisha na kuonekana kuwa bado kuna wachezaji wengi kwenye Ligi Kuu hawafanyi kazi zao sawa sawa.

Kwenye orodha hiyo, kuna wachezaji ambao walitakiwa kuwamo wenye namba zao, lakini hawamo, ila yupo Djuma Shaaban, beki wa kulia wa Yanga ambaye ana 'assist' nne, na viungo washambuliaji wa Azam, Tepsi Evance, Aboubakar Ngalema wa Dodoma Jiji, pamoja na Chiristian Zigah wa Biashara United.

Ikumbukwe kuwa Zigah ni Raia wa Ghana na Djuma ni Mkongomani. Hawa wanastahili sifa kwa sababu wameifanya kazi yao sawasawa kuliko wengine ambao hawamo, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa idadi hiyo bado ni ndogo.

Kama kuna makocha wanakuja kufanya tathmini na kugundua hili ni kwamba tutarajie sasa misimu inayofuata, mabeki wa pembeni na viungo washambuliaji nao wanaweza kusajiliwa kutoka nje ya nchi. Ni kwa sababu wachezaji wa Kitanzania wanaonekana bado hawafanyi kazi yao vizuri. Itakuwa ni hatari kwa sababu wachezaji wa Kibongo wameanza kupoteza nafasi zao kwenye ushambuliaji, na taratibu inaelekea kwenye mabeki wa kati.

Hakuna kocha ambaye anaweza kuvumilia kukaa na mabeki wa pembeni na viungo washambuliaji ambao kwa msimu wanatoa 'assist' nne, tano au sita.

Kwa misimu miwili kiungo wa Simba, Clatous Chama ndiye aliongoza kwa kupiga pasi za mwisho.

Msimu wa 2019/20 alimaliza ligi akiwa na 'assist' 10, na msimu uliopita alivunja rekodi yake mwenyewe kwa kumaliza na 'assist' 11, huku mchezaji mwingine wa kigeni Luis Miquissone akiwa nazo tisa. Inaonyesha kuwa Chama kama angeanza tena msimu huu tangu mwanzo, angeweza kuwa kinara kwa mara nyingine tena. Kwa nini iwe yeye tu?

Hapa ndipo tunarudi nyuma kama taifa tutengeneze wachezaji wetu wakiwa bado makinda. Wawe na makocha wenye uwezo mkubwa na siyo wanakuja kupata makocha wenye uwezo mkubwa wakiwa Ligi Kuu, jambo ambalo wanakuwa hawabadiliki.

Kwa hali hii sasa, si mastraika tu, hata 'maassist' sasa watakuwa wanasajiliwa kutoka nje ya nchi.

# Madereva malori wanaobeba abiria kukiona

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Kamishna Msaidizi wa Polisi (SACP) Wilbrod Mutafungwa, ametangaza kiama kwa madereva wa magari ya mizigo (malori) wanaosafirisha abiria kutoka sehemu moja kwenye nyingine kwa kuwa hairuhusiwi kisheria.

Mutafungwa alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki muda mfupi baada ya kufanya ukaguzi wa magari ya abiria na mizigo wakati wa operesheni ya kudhibiti makosa na kuzuia ajali za barabarani.

Alisema magari makubwa ya mizigo yanayofanya safari ndani na nchi jirani, madereva wake wamekuwa na tabia ya kubeba abiria pasipokuwa na leseni za usafirishaji wa watu.

Aliongeza kuwa inapotokea ajali unakuta idadi ya vifo inakuwa kubwa katika magari hayo licha ya kuwa hayatakiwa kubeba abiria. "Magari ya mizigo hayaruhusiwi kubeba abiria badala yake yaliyoruhusiwa kufanya kazi hiyo ni mabasi ambayo yana leseni ya usafirishaji wa abiria," alisema.

Mutafungwa alisema katika operesheni hiyo wanatumia vifaa vya kudhibiti mwendo kasi, mifumo ya ukaguzi, vipimo vya kupima ulevi pamoja na mipango kazi dhabiti ya askari ya ukaguzi wa mara kwa mara na dereva anayeonekana kuwa sugu wa makosa atafungiwa kuendesha chombo cha moto.

Aidha, alisema magari mengi yamekuwa yakipata ajali kutokana na mambo mbalimbali ikiwamo ulevi, mwendo kasi wa magari hayo huku abiria wengi wakikubaliana na hali hiyo.

Alisema kwa sasa matunda yameanza kuonekana kutokana na elimu ya usalama barabarani inayotolewa nchi nzima na askari wake na kwamba madereva wengi wamebadilika hivyo kuleta matumaini katika kupunguza ajali kwa kiasi kikubwa.

Mutafungwa alisema katika operesheni iliyofanyika Wilaya ya Gairo mkoani Morogoro na Kanda ya Ziwa, mabasi 173 yalikaguliwa kati ya hayo 87 yalifuata utaratibu wa usalama barabarani, 47 yalitozwa faini, tisa waliaonya, magari manane yalikuwa yamezima ving'amuzi na mengine yakiwa hayana breki na matairi kuwa vipara.

Alifafanua kuwa magari 15 yalikuwa mabovu na yalikuwa yamebeba abiria na waliyazuia kuendelea na safari mpaka pale yatakapotengenezwa na kukaguliwa na askari. Aliongeza kuwa hawatawavumilia madereva sugu ambao watakamatwa kwa makosa ya kutotii alama za barabarani.

Mmoja wa madereva wa magari makubwa yaendayo nchi jirani ya Rwanda, Omary Juma, alikiri kuwapo kwa baadhi ya magari ya mizigo kubeba abiria.

Dereva mwingine, William Mashamba, alisema wanaokuwa na tabia ya kubeba abiria katika magari hiyo ni madereva wa kitanzania, lakini wenzao kutoka nchi jirani hawana tabia hizo kwa sababu sheria zinawabana.



Muuguzi wa Kituo cha Afya cha Kampuni ya Sukari ya Kilombero, akitoa chanjo ya UVIKO-19 kwa mmoja wa wananchi waliojitokeza kupata huduma wakati wa upimaji afya na utoaji chanjo ulioandaliwa na kampuni hiyo katika kuadhimisha Siku ya Wauguzi Duniani, Mei 12, wilayani Kilombero, mkoani Morogoro. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Umilikishaji ardhi kuwakomboa wanawake

**Anthony Ishengoma na Munir Shemweta,** MBEYA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amesema faida kubwa na kipaumbele katika kupanga, kupima na kumilikisha ardhi ni kupambana na ukatili dhidi ya wanawake ikiwamo kuondoa changamoto ya kukosa nguvu ya kumiliki ardhi.

Kikwete amesema hali hiyo itapatikana kwa kutoa hati ya pamoja ya umiliki ardhi kati ya mume na mke.

Alisema hayo juzi wakati akihutubia wananchi wa Mbalizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wakati wa uzinduzi wa mradi wa kupanga, kupima na kumilikishwa ardhi unaosimamiwa na Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) na baadaye kushiriki ugawaji hati kwa wananchi waliokamilisha taratibu za kumilikishwa ardhi.

Aliongeza kuwa kupima ardhi kutawezesha kutatua migogoro isiyo ya lazima kwa kuwa kazi hiyo inahusisha upimaji shirikishi ambao baada ya wataalamu kujiridhisha, hati hutolewa bila migogoro yoyote.

"Kumekuwapo na spidi (kasi) ndogo ya wananchi kwenda kuchukua hati zao lakini niwaambie ninyi kuna wakati utafika mtahitaji kulima kadiri ya taratibu za serikali na kuepuka uharibifu wa mazingira. Kuna wakati itabidi zitumike mbinu za kitaalamu ili kuendelea na kilimo," alisema.

Naibu Waziri alizitaja faida za kuwa na hati kuwa ni pamoja na kuthaminiwa na kupatiwa uhakika wa huduma za kibenki kwa mmiliki, kuongeza thamani ya ardhi tofauti na ardhi isiyopimwa aliyoieleza kuwa haina thamani yoyote nchini.

Mkuu wa Chuo Ardhi Morogoro (ARIMO), Huruma Lugalla, alisema chuo kilikopeshwa Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya programu ya kupima, kupanga na kumilikisha ardhi kwa wakazi wa Mbalizi na viwanja takribani 35,000 vimepimwa.

Kwa mujibu wa Lugala, kiasi hicho cha fedha kimewezesha upimaji na utambuzi wa viwanja 31,06 sawa na asilimia 89 katika lengo lililokusudiwa.

Pia alisema upimaji wa viwanja hivyo ulikwenda sambamba na uandaaji wa michoro ya mipango miji na tayari michoro 108 kati ya 120, sawa na asilimia 90 imesanifiwa na kati ya hiyo, 80 imewasilishwa ofisi ya Kamishna wa Ardhi wa Mkoa kwa ajili ya idhini.

Naibu Waziri Kikwete ambaye amehitimisha ziara yake ya siku mbili mkoani Mbeya, alisema zaidi ya Sh. bilioni tatu zimefika katika mkoa huo kwa lengo la kupima, kupanga na kumilikisha ardhi na kusimamiwa vizuri na watendaji wa serikali na kukabidhi hati kwa wananchi wa Mbalizi waliokamilisha taratibu za kumilikishwa ardhi.

## 800 wapatiwa huduma za afya

**Na Mary Geofrey**

KAMPUNI ya Sukari ya Kilombero, imetoa huduma ya matibabu bila malipo ikiwamo chanjo ya UVIKO-19 kwa wananchi 800 wanaoishi ndani na nje ya eneo la kiwanda hicho.

Huduma hiyo ilitolewa na kampuni hiyo, kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wauguzi Duniani ambayo huadhimishwa kila mwaka Mei 12 na kaulimbiu ilikuwa ikisema, 'Wauguzi: Sauti Inayoongoza - Wekeza kwenye Uuguzi na Heshimu Haki ili Kulinda Afya kwa Wote'.

Akizungumza wakati wa kutoa huduma hiyo, mwisho mwa wiki, daktari wa zamu katika kituo hicho cha afya, Dk. George Komba, alisema huduma zilizotolewa ni huduma za uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi na saratani ya matiti, uchunguzi wa shinikizo la damu la juu na elimu ya kuzuia na kudhibiti shinikizo la damu la juu.

Huuduma zingine zilizotolewa ni tohara kwa wanaume wenye miaka 15 na zaidi, upimaji wa virusi vya UKimwi (VVU) na ushauri nasaha, na huduma za uzazi wa mpango kama vile vipandikizi na vitanzi.

"Tunatambua mchango wa wauguzi katika jamii, hivyo tuliandaa kampeni hii, ili kuungana na wauguzi wetu katika kusherehekea siku hii maalum na kudhihirisha umuhimu wao katika jamii kupitia zoezi hili la upimaji afya," alisema.

"Tuliamua kusherehekea Siku ya Wauguzi Duniani kupitia upimaji afya kwani tunatambua umuhimu wa wadau wote kuchangia katika kupunguza magonjwa ambayo yanaweza kuzuilika kupitia chanjo na uelewa wa masuala ya afya. Pia tulitaka kutoa ahueni kwa watu wenye uwezo mdogo wa kupata huduma za afya kutokana na umaskini au uelewa mdogo kuhusu masuala ya afya," alisema.

Naye Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa kampuni hiyo, Willa Haonga, alisema wapo mstari wa mbele kuchangia upatikanaji wa huduma za kijamii kwenye jamii.

Alisema kituo cha afya cha kampuni hiyo kinahudumia zaidi ya wagonjwa 2,700 kwa mwezi na asilimia 50 ni wanaotoka vijiji vya jirani.

Kituo hicho cha afya hutoa huduma bure kwa wafanyakazi wa kampuni na kutoza gharama ndogo kwa wakazi wanaoishi katika vijiji vinavyozunguka kiwanda hicho.




Zarina Hassan maarufu Zari 'The Boss Lady' akiwa pamoja na wanafunzi wa shule za sekondari zilizoko wilayani Misungwi mkoani Mwanza, baada ya kutoa taulo za kike katika shule za msingi 150 na sekondari 32 za serikali wilayani humo. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel. **PICHA: ROSE JACOB**

# Watumishi waliosimamishwa kazi warejeshwa kazini

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

WATUMISHI 14 kati ya 16 wa Halmashauri ya Mji wa Masasi ambao walisimamishwa kazi kutokana na tuhuma mbalimbali zikiwamo utovu wa nidhamu kazini na ubadhirifu wa fedha, wamerejeshwa kazini.

Pamoja na kurejeshwa kazini, wamepewa masharti ya kulipa fedha kwa kukatwa asilimia 15 ya sehemu ya mishahara yao kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo.

Uamuzi huo ulitolewa mwishoni mwa wiki mjini hapo kupitia kikao cha Baraza la Madiwani la Halmashauri hiyo baada ya kujadili kisha kutoa maazimio ambayo yalipewa baraka zote na wajumbe wa kikao hicho.

Akitangaza uamuzi huo, Mwenyekiti wa Halmashauri ambaye ni Diwani wa Jida, Hashim Namtumba, alisema kikao hicho cha baraza katika kujadili taarifa za watumishi, kimejadili taarifa nne zinazowahusu watumishi 16 kati ya watumishi hao 14 ambao walisimamishwa kazi miezi kadhaa iliyopita.

Namtumba alisema katika mashauri hayo yanayowahusu watumishi ambao walikuwa na mashauri mbalimbali yakiwamo utovu wa nidhamu kazini, ubadhirifu wa fedha na makosa ya kiutumishi, watumishi wawili kati yao wao wamefukuzwa kazi kutokana na ukubwa wa makosa yao na wajumbe kushindwa kuwasamehe.

Alisema licha ya watumishi hao kupewa adhabu hiyo ya kusamehewa kwa masharti, wako wengine ambao wamerejeshwa kazini kwa kusamehewa bila kupewa adhabu ya aina yoyote kutokana na kutokutwa na hatia yoyote katika mashauri yao.

"Adhabu hizi baraza limezitoa kupitia sheria za utumishi wa umma na si kama baraza limeajiamulia. Bazara limekaa na kujadili makosa ya watumishi hawa kupitia sheria hizi za utumishi wa umma," alisema Namtumba.

Alisema katika jambo hilo, watumishi wawili wamefukwa kazi kutokana na makosa yao kutosameheka, hivyo baraza kuamua kutoa uamuzi wa kuwafukuza moja kwa moja na kwamba hiyo itakuwa fundisho kwa watumishi wengine ambao watafanya tabia kama walizofanya watumishi hao. Namtumba aliwataja baadhi ya watumishi hao kuwa ni Ofisa Mipango, Abirahi Mfinanga ambaye yeye hakukutwa na hatia yoyote hivyo baraza limeamua kumsamehe bila ya masharti, Henri Amani aliyekuwa mweka hazina anakatwa asilimia 15 ndani ya miaka mitatu, Changwesi Kajele ambaye amerejeshwa bila ya masharti na Asina Marumbwe ambaye ni mtumishi kitengo cha ununuzi atakatwa asilimia 15.

Wengine kwa mujibu wa Namtumba ni Renard Mkondola ambaye amesamehewa bila masharti, Jamadi Kasimba mtendaji kata ya Mkuti, amepewa adhabu ya kukatwa asilimia 15 ya mshahara wake kwa kipindi cha miaka mitatu.

Alisema watumishi wengine ambao pia wamekumbana na adhabu hiyo ni Zuhura Ngalinje na Hashimu Chiwaya ambao wote wawili ni kutoka idara ya afya na Michael Evarist ambaye baraza limeamua kumfukuza kazi kutokana na makosa yake kutosamehewa.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, alisema watumishi wanapaswa kufanya kazi kwa uaminifu na kuheshimu misingi ya kazi zao ambazo zinazongozwa na sheria za utumishi wa umma.

# Kampuni ya Tanzania yashinda tuzo Afrika

**Na Jenifer Gilla**

KAMPUNI ya Kitanzania inayojishughulisha na kutoa mikopo, Laina Finance, imepata tuzo ya ubora Afrika inayotoa huduma ya malipo ya simu, katika mashindano yaliyoandaliwa na kampuni ya VIVA tech inayoandaa maonyesho makubwa ya teknolojia barani Ulaya.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Biashara wa kampuni hiyo, Tonny Missokia, alisema walishiriki mashindano hayo baada ya kutangazwa mwanzoni mwa mwaka huu na kushirikisha zaidi ya 90.

"Walitangaza shindano la kutafuta kampuni inayotoa huduma bora katika ununuzi wa njia ya simu ya malipo kwa njia ya awamu.

Walitangaza Afrika nzima na walipata washiriki zaidi ya 90 pamoja na Laina Finance na tukachaguliwa kuwa ni kampuni bora Afrika," alisema Missokia.

Alisema kilichofanya kampuni hiyo kuibuka na ushindi ni urahisi wa teknolojia yake na jinsi inavyoweza kuhudumia watu wa maeneo mbalimbali kupata kukidhi mahitaji yao.

Kutokana na ushindi huo, alisema kampuni hiyo itaiwakilisha Tanzania katika maonyesho makubwa ya teknolojia na ubunifu yatakayofanyika nchini Ufaransa mwezi ujao pamoja na kuitangaza kampuni hiyo kwenye soko la kimataifa.

"Tumeona ni habari njema basi tuwataarifu Watanzania na wadau tunaoshirikiana nao katika kuihudumia jamii kupitia kuwawezesha kukopa vitu mbalimbali ili kuwasaidia kutimiza matakwa yao," alisema.

Alisema kwa sasa wanafanya kazi na kampuni ya Vodacoma na Hisense na Samsung ambazo mtu anaweza kuchukua mkopo wa simu na vifaa vya ndani kama vile Tv na friji kisha akalipa kwa awamu.

"Mteja akishatimiza vigezo na masharti yetu anakwenda kwenye duka la vodacom au hayo niliyoyataja, anachukua kitu anachokihitaji kisha analipa kiasi kidogo cha mkopo, kilichobakia tunakilipa sisi kwa kampuni halafu tunamkata yeye kidogo kidogo," alifafanua.

Kwa mujibu wa Missokia, tangu kuanzishwa mwaka 2018 mpaka sasa, kampuni hiyo imeshawafikia na kuwahudumia Watanzania takribani 10,000 na malengo yao ni kuwafikia zaidi ya hao na kupanua wigo wa kutoa huduma.

"Malengo yetu si tu kuishia kwenye mikopo ya vitu vya umeme tunataka tuwezeshe Watanzania kukupa bidhaa mbalimbali za madukani ikiwamo vyombo, pembejeo, dawa, vifaa tiba na hata vifaa vya ujenzi," alisema.

# Wanawake washauriwa kusaidia watoto yatima

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

WANAWAKE mkoani Rukwa wameshauriwa kuwa na moyo wa huruma na kujitolea kuwasaidia watoto yatima wanaolelewa katika vituo mkoani mkoani hapa kwa kuwa wanajua uchungu wa watoto hasa waliofiwa na mama zao katika umri mdogo.

Ushauri huo ulitolewa jana na Jasmin Simba, Mwenyekiti wa Taasisi ya Wanawake ya Itambue Thamani Yako (ITY) inayojishughulisha kutoa misaada kwa watu wenye uhitaji.

Taasisi hiyo jana ilitoa misaada kwa watoto yatima wanaolelewa katika Kituo cha Mtakatifu Martine De Pores mjini hapo.

Alisema wanawake ni watu wenye huruma na wanajua vizuri changamoto walizo nazo watoto hasa wale ambao mama zao wamefariki dunia na kuwaacha wachanga, hivyo wanapaswa kuwa wa kwanza kuwasaidia kwa kujitolea kwa hali na mali.

Alisema taasisi hiyo ina wanachama ambao ni wanawake tu, ambayo ipo mkoani hapa, hivyo waliamua kuchangishana na kutoa misaada mbalimbali yenye thamani ya Sh. 550,000 pamoja na kuandaa chakula cha mchana na kula nao watoto hao.

Naye Katibu ITY, Debora Gwakisa, alisema walipofuatilia taarifa za watoto walioko katika kituo hicho, walibaini kuwa wana changamoto nyingi ambazo jamii inapaswa kushughulikia ndiyo maana waliamua kuchangishana na kupata kiasi hicho cha fedha na kwenda kuwasaidia.

Alisema kwa niaba ya wanachama wenzake wanawaomba wanawake walioko katika maeneo tofauti nchini kuwa na utamaduni wa kuwatembelea na kuwasaidia watoto yatima wanaolelewa katika vituo pamoja na wale wanaoishi katika mazingira magumu kwa kuwa wana uhitaji wa mambo mengi lakini wamekuwa wakiyakosa.

Sista Agness Mwananjera ambaye ni mlezi mdogo wa watoto katika kituo, alisema kuwa kituo hicho kinakabiliwa na changamoto nyingi ikiwamo uwezo mdogo wa kununua umeme, tangi la maji limepasuka na lililopo halikidhi mahitaji, baadhi ya watoto hawana bima za afya, wanahitaji mashuka na mablanketi na mahitaji mengine mengi.

Aliwashukuru wanawake hao kwa moyo wao wa upendo wa kufika katika kituo hicho kinachomilikiwa na Kanisa Katoliki na kuwataka kuwa mabalozi kwa kuwaeleza wananchi wengine hususani wanawake ili waone umuhimu wa kuwasaidia watoto hao.

## ‘Mitazamo hasi kwa mwanamke iepukwe’

**Na Christina Haule,** MOROGORO

JAMII ya kitanzania imetakiwa kujiepusha na mitazamo hasi na kumruhusu mwanamke kufanya Usimamizi wa Shughuli za Misitu ya Jamii (USMJ) ili kuleta mabadiliko chanya kwa kunufaika na rasilimali misitu.

Hayo yalisemwa na ofisa wa kujengea uwezo kutoka Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania (TFCG), Simon Lugazo, wakati wa warsha ya wadau wa Jukwaa la Vyama vya Kiraia na Watu Binafsi wanaofanya kazi za kuboresha misitu kwa manufaa Tanzania (TFWG) juu ya masuala ya usawa wa kijinsia kwenye shughuli za misitu.

Lugazo alisema ingawa hakujakuwa na idadi ya sawa kwa wanawake na wanaume, wanawake wameamka katika suala la umiliki wa ardhi, kufanya biashara za misitu na kushiriki katika vikundi vya hisa kupitia VICOBA vilivyoanzishwa kutoka kwenye faida za rasilimali za misitu.

Alisema wako wanaume wenye mitazamo tofauti na kuona kuwa shughuli za misitu ni za wanaume pekee na kusahau kuwa ziko zingine zinazoweza kufanywa na wanawake ikiwamo kuwauzia chakula wanaume wanaokata miti na kuchoma mkaa.

Awali, Mtafiti wa Masuala ya Jinsia kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Emmanuel Mroto, alisema wako wanawake ambao kwa sasa wameanza kujishughulisha na ukataji mkaa na kufungua miradi mbalimbali huku akishauri pia vijana nao kuhamasishwa vya kutosha kushiriki katika mradi.

Mmoja wa washiriki wa warsha hiyo, Isaya Sekibo, kutoka SUREDO alisema miongoni mwa shughuli kubwa wanazozifanya ni kuhakikisha wanawake wanashirikishwa na wanashiriki vya kutosha katika shughuli za misitu tofauti na awali.

Warsha hiyo ambayo imehusisha wadau wa TFWG imewezeshwa na mradi wa kuhifadhi misitu kupitia biashara endelevu ya mazao ya misitu (CoFoReST ) unaoendeshwa na TFCG wakishirikiana na MJUMITA kwa ufadhili wa Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC).



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya (kushoto), akiteta jambo na viongozi wa Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB), alipokwenda kufunga mkutano wa mashauriano wa makandarasi wa ndani uliofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dodoma. Anayefuata ni Mwenyekiti wa CRB, Mhandisi Consolata Ngimbwa, Makamu Mwenyekiti Joseph Tango, Msajili wa CRB, Mhandisi Rhoben Nkori na Msajili Msaidizi, David Jere. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali yawataka makandarasi kuungana kupata miradi mikubwa

**Na Joseph Mwendapole,** DODOMA

SERIKALI imewashauri makandarasi wa ndani waungane ili waweze kufanya miradi mikubwa inayochukua fedha nyingi hali itakayosababisha fedha nyingi za ujenzi kubaki hapa nchini.

Wito huo ulitolewa mwishoni mwa wiki jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Godfrey Kasekenya, alipokuwa akifunga mkutano wa siku mbili wa mashauriano kwa makandarasi wazawa ulioandaliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB).

Alisema kwa sasa asilimia karibu 70 ya fedha za miradi ya ujenzi zinakwenda kwa kampuni kubwa za nje ya nchi wakati fedha hizo zingeweza kubaki nchini iwapo makandarasi wangekuwa na nguvu ya kufanya kazi hizo.

“Mkifanya nyinyi tutawalipa na fedha hizo zitabaki kenye mzunguko wa uchumi wetu hapa tofauti na sasa ambapo fedha nyingi za miradi ya ujenzi zinakwenda nje ya nchi. Jambo hili si zuri sana kwa uchumi wetu ndiyo maana tunaomba muungane mpate nguvu ya kufanya miradi hiyo,” alisema.

Naibu Waziri pia aliwataka watoa zabuni za ujenzi kuwalipa makandarasi kwa wakati ili wafanye kazi zao kwa ufanisi badala ya kuwarushia lawama kwamba wanachelewesha miradi wakati hawajawalipa.

Alisema ametembelea miradi mingi ya ujenzi na kubaini kuwa baadhi ya waajiri hawatimizi wajibu wao wa kuwalipa makandarasi kwa wakati lakini wamekuwa wakiwaangushia lawama kwamba wanachelewesha.

“Natoa wito kwa waajiri na watoa zabuni wote kuhakikisha wanazingatia mikataba yao ili kama wanataka kazi iende kwa wakati basi na wao watimize wajibu wao wa kuwalipa makandarasi kulingana na mikataba waliyoaingia,” alisema Naibu Waziri.

Hata hivyo, Naibu Waziri aliwageukia makandarasi hao kuwataka wahakikishe wanatimiza wajibu wao kwa kukamilisha miradi kwa wakati na kwa viwango vinavyotakiwa kwa mujibu wa mkataba wanapolipwa fedha za ujenzi.

“Iko miradi mnafanya lakini kwa kweli viwango si bora. Sasa fanyeni kazi ili mtu aone thamani ya fedha alizotoa. Usilipue kazi ya watu mpaka mtu akajuta kwa nini amekupa kazi yake. Kwa hiyo mwajiri anapaswa kutimiza wajibu wake na wewe mkandarasi timiza ajibu wako,” alisema.

Naibu Waziri aliwataka pia makandarasi kuihusisha Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ili kuwashauri wakati gani mzuri wa kuanza ujenzi kwa kuwa vinginevyo wanaweza kujiingiza kwenye hasara kubwa.

Msajili wa Bodi ya Makandarasi (CRB), Mhandisi Rhoben Nkori, alisema makandarasi wa ndani wamezungumzia upendeleo kwenye baadhi ya maeneo na uchache wa miradi ya kuwajengea uwezo.

Alisema wengi wamezungumzia changamoto ya kucheleweshewa malipo na watoa zabuni wengi zikiwamo wizara, taasisi za umma na sekta binafsi hali ambayo inawakwamisha kufanya kazi kwa ufanisi.

Mhandisi Nkori alisema maazimio mengine ni ya kuwataka wanasiasa kuacha kuwadhalilisha makandarasi kwa kuwaweka ndani na wakati mwingine kuwadhalilisha kwenye vyombo vya habari bila kufuata taratibu.

“Wamesema kuna wakati viongozi wanapotembelea miradi na kubaini mapungufu wanaona ni makosa ya mkandarasi wanaiweka kwenye vyombo vya habari bila kuangalia mkataba unasemaje na hali hiyo inaifanya kazi ya ukandarasi kuonekana kama ya ubabaishaji,” alisema.

# Jitihada kuongezwa mapambano dhidi ya ukatili

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kuongeza jitihada katika mapambano dhidi ya vitendo vya ukatili kwa wanawake na watoto ili kuhakikisha makundi hayo yanakuwa salama nchini.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu, Dk. John Jingu, aliyasema hayo jana kwenye kikao cha kamati elekezi ya mpango kazi wa Taifa wa kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) kilichofanyika jijini Dodoma.

Alisema kuwa ipo haja ya kuongeza nguvu katika mapambano hayo kila mdau kwa nafasi yake ili kuongeza jitihada za utekelezaji wa mpango huo kutokana na kuongezeka kwa vitendo na matukio ya ukatili katika maeneo mbalimbali.

Dk. Jingu alisema serikali kwa kushirikiana na sekta mbalimbali za maendeleo itaongeza nguvu ili kulinda na kuwatetea makundi hayo ya watoto na wanawake ambayo imekuwa wakikosa usalama wao.

“Inabidi tuongeze nguvu yaani serikali, wizara za kisekta idara, taasisi, asasi za kiraia, wadau na vyombo vya ulinzi katika mapambano haya wote kwa nafasi zetu ili kuongeza kazi ya utekelezaji wa mpango huu na kufikia hilo lazima tuwe na rasilimali kulinda na kutetea makundi ambayo yamekuwa yakiathirika kutokana na vitendo hivyo,” alisema Dk. Jingu.

Katibu Mkuu huyo alisema kwa mujibu wa mwongozo wa maandalizi ya mpango na bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2022/23 unaelekeza kutengwa kwa fedha kwa ajili ya kutekeleza afua za MTAKUWWA huku akiziomba taasisi na wadau kuona namna ya kuongeza rasilimali ili kufikia malengo ya kukomesha vitendo vya ukatili.

“Niwaombe wenzetu ambao ni wadau wa maendeleo na asasi za kiraia nimewaomba tuongeze rasilimali katika vita hii kwa sababu inahitaji ushirikiano wa pamoja kwani inamgusa kila mmoja wetu katika jamii zetu,” alisema.

Naye Mtaalamu wa Masuala ya Usalama wa Mtoto kutoka Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF), Violet Mollel, alisema wamekuwa wakitoa elimu kwa wana jamii namna ya kudhibiti vyanzo vya ukatili.

Mollel aliahidi shirika hilo bado litaendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika uandaaji wa mkakati mpya wa 2022 hadi mwaka 2027 pamoja na kuratibu kamati za ulinzi kuanzia ngazi ya vijiji hadi mkoa.




Mkurugenzi wa M-pesa, Epimack Mbeteni (kulia), Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jubilee Insurance, Dinpankar Acharya (kushoto), Meneja wa Utekelezaji Sheria na Kushughulikia Malalamiko (TIRA), Okoka Mgavilenzi (watatu kulia), Ofisa Bima Mkuu Mo Assurance, Pamela Ndosi (wapili kushoto), Mkuu wa Kitengo cha Mauzo Milvik, Ismail Simanga (watatu kushoto), wakiwa pamoja katika uzinduzi rasmi wa huduma ya VodaBima "Linda Afya na VodaBima". **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Washauriwa kutoficha watoto wenye ulemavu

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZAZI na walezi mkoani Shinyanga ambao wanaishi na watoto wenye ulemavu, wametakiwa kutowaficha bali wawapatie haki yao ya kielimu na kutimiza ndoto zao, kama watoto wengine wasio na ulemavu.

Mratibu wa kikundi cha WhatsApp Together We Fight, Gwakisa Mwasyeba, alibainisha hayo juzi wakati wanakikundi walipotembelea kituo cha kutoa elimu kwa watoto wenye mtindio wa ubongo cha Brothers of Charity kilichoko Kitangili Manispaa ya Shinyanga, na kutoa misaada ya vitu mbalimbali kikiwamo chakula.

Alisema wamefarijika kuona watoto wenye mtindio wa ubongo wakipata elimu, na kutoa wito kwa wazazi na walezi mkoani Shinyanga ambao wanaishi na watoto wenye ulemavu wasiwafiche ndani, bali wawapeleke shule na kupata elimu ili kutimiza ndoto zao.

"Kikundi chetu cha WhatsApp, tumeguswa na watoto hawa wenye mtindio wa ubongo, na kuamua kuchangisha fedha Sh. 10,000 kwa kila mwanakikundi, na kununua vitu mbalimbali kikiwamo chakula na kukileta hapa kituoni, ili watoto hawa wasome wakiwa na furaha," alisema Mwasyeba.

Alitaja vitu ambavyo wamevitoa kwa watoto hao kuwa ni mchele kilo 200, unga wa mahindi kilo 100, madaftari makasha mawili, juisi, pipi, sabuni za unga, za mche, biskuti, chumvi, dawa za meno, penseli na nguo.

Mkuu wa Kituo cha Brothers Charity, George Rice, alikishukuru kikundi hicho cha WhatsApp kwa kuguswa na watoto hao na kuwapatia msaada, na kutoa wito kwa wanavikundi wengine kuiga mfano huo.

# Viongozi dini waombwa kuhamasisha sensa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel, amewaomba viongozi wa dini kuhamasisha wananchi kushiriki ipasavyo sensa ya watu na makazi itakayofanyika Agosti 23, mwaka huu.

Akizungumza jana kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, kwenye ufunguzi wa Ofisi Kuu ya Kanisa la Evangelistc Assemblies of God Tanzania (EAGT) Ilazo Dodoma, Emmanuel aliomba viongozi wa dini kutumia nafasi zao kuwapa elimu waumini ili kutoa taarifa sahihi kuhusu sensa hiyo.

Alisema kuwa serikali kupitia sensa, itatambua idadi ya watu wake ili kupanga bajeti itakayowagusa Watanzania wote na hatimaye kuhudumiwa.

Kwa mujibu wa mkuu huyo wa wilaya, serikali bado itaendelea na kudhamini juhudi kubwa zinazofanywa na taasisi za kidini katika uwekezaji wa miundombinu mbalimbali inayofanywa.

Alisema kuwapo kwa majengo ya vyuo vikuu vya elimu vya kiroho ni sehemu kubwa ya mchango katika kuisaidia watu wake kupata elimu iliyo sahihi.

"Vijana wasomi wanatakiwa kutumia elimu na taalamu wanazozipata kupitia vyuo hivyo vya kiroho kwa manufaa ya kujenga nchi ya kimaendeleo ikiwamo na kumtumikia Mungu," alisema.

Askofu Mkuu wa Kanisa hilo, Brouwn Mwakipesile, alisema kanisa litaendelea kuunga mkono juhudi mbalimbali zinazofanywa kwa ajili ya taasisi za kidini.

Alisema mafanikio ambayo kanisa hilo yamefikiwa ni pamoja na waumini wake kuwa na moyo wa kujitoa katika kuchangia shughuli mbalimbali zinazohusu wao wenyewe katika maendeleo badala ya kutegemea wafadhili wa kutoka nje.

Alitaja mafanikio hayo ni pamoja na uwezeshaji wa ujenzi wa ofisi kuu ya kanisa hilo umegharimu Sh. milioni 282.

# RC atangaza msako wahusika ukatili

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, ametangaza msako dhidi ya watu wanaojihusisha na vitendo vya ukatili ndani ya mkoa.

Akizungumza jana wakati wa Siku ya Familia Duniani, Sendiga alisema mkoa wa Iringa umejiwekea mikakati kabambe ya kukomesha matukio ya ukatili yanayojitokeza kwenye jamii na kutaka wananchi wasikubali kufumbia macho vitendo vyovyote vya ukatili kwenye maeneo yao.

Sendiga alisema kutokana na elimu inayoendelea kutolewa dhidi ya ukatili ndani ya mkoa, idadi ya wanaume wanaofika dawati la jinsia kulalamika kufanyiwa ukatili na wake zao imeongezeka tofauti na mwanzo.

Alisema wanaume awali walikuwa wakiona aibu kwenda polisi kutoa taarifa za wao kufanyiwa ukatili na wanawake.

"Tunapoona wanaume wanajitokeza kwenda kulalamika kufanyiwa vitendo vya ukatili, tunaamini elimu imefika na ni mwanzo mzuri wa matukio ya ukatili kuendelea kupungua mkoani kwetu," alisema.

Hata hivyo, alisema bado ukatili dhidi ya wanawake na watoto umeendelea kuwapo japo si kwa kasi kubwa kama zamani na kutaka jamii kuendelea kuwaibua wanaofanya ukatili.

Mkuu wa mkoa alisema iwapo wazazi watazingatia ushauri mbalimbali unaotolewa na viongozi wa serikali na vyombo vya usalama kuhusu uangalizi wa watoto, itasaidia kupunguza kabisa matukio ya ubakaji, ulawiti na mengine kwa watoto nyakati za usiku.

Alisema vitendo vya baadhi ya wazazi au walezi kuwatuma watoto usiku kwenye maduka ni moja ya sababu zinazochochea ubakaji na ulawiti kwa watoto.

Katika hatua nyingine, mkuu huyo wa mkoa alisema ukatili wa baadhi ya wanaume hasa wanaolewa kupindukia kunyonya maziwa ya wake zao wanaonyonyesha kwa imani ya kukata pombe, unaendelea kupungua na kuwashauri wanaume hao kuacha tabia hizo.

Nipashe

# Spotika



WACHEZAJI AMBAO HAWAJAUTENDEA HAKI MSHAHARA WAO EPL UK. 12-13

# SABABU 5 KWA NINI UNITED HAIPASWI KUMUUZA RONALDO



**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo amekuwa mmoja wa wachezaji wachache wazuri katika msimu huu ambao umekuwa wa kukatisha tamaa kwa Manchester United.

Man United wako tayari kufanyia kikosi chao marekebisho makubwa msimu huu wa majira ya joto. Kocha mpya Erik ten Hag atachukua usukani mwishoni mwa msimu huu na atatumaini kuunda timu ambayo inaweza kuleta changamoto.

Kwa mujibu wa Mwandishi wa Habari wa Ureno, Pedro Almeida, Ronaldo anaweza asiwe sehemu ya mipango ya Hag kwa msimu wa 2021-22. Lakini je, kumtoa mchezaji ambaye amefanya vema katika muda wote wa msimu ni uamuzi unaofaa kwa klabu?

Hebu tuangalie sababu tano kwa nini Man United hawapaswi kumuuza Ronaldo msimu huu wa majira ya joto, twende sasa...

**#5. Ronaldo amekuwa bora kwa Man United**

Ronaldo bila shaka amekuwa mchezaji bora wa Man United msimu huu. Amewasilisha mara kwa mara na ametoa mchango mwingi wakati wakishinda mechi msimu huu.

Amefunga mabao 24 na kutoa pasi tatu za mabao katika mechi 37 alizocheza kwenye michuano yote akiwa na Man United hadi sasa msimu huu. Alikaribia kuisaidia timu yake kufuzu kwenye mtoano kutoka hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#4. Kiwango kizuri hatua za mwisho za msimu**

Moja ya shutuma kuu zilizowasilishwa dhidi ya Man United kwa kumrejesha Ronaldo kwenye klabu msimu uliopita ni umri wake. Akiwa na umri wa miaka 37, Ronaldo anaonekana yuko kwenye 'mwisho' wa kazi yake, lakini hachezi kama hivyo.

Kwa mwenye umri wa miaka 37, Ronaldo ameonyesha kiwango cha ajabu na kuvutia. Pia ameongezeka katika miezi ya hivi karibuni na amekuwa katika kiwango kizuri cha ufungaji. Ronaldo pia amefanya kazi katika uchezaji wake wa kiungo na kuboresha mchango wake wa ulinzi pia.

Katika mechi sita za mwisho za Ligi Kuu England akiwa na Man United, Ronaldo amefunga mabao tisa. Itakuwa hasara kubwa kwa 'Mashetani Wekundu' hao ikiwa hawatakuwa naye msimu ujao.

**#3. Anafaa wakati wa kuunda upya kikosi**

Ronaldo ameshinda karibu kila kitu kwenye ulimwengu wa soka. Ni mmoja wa wachezaji bora zaidi wa wakati wote, na bado anaendelea kuimarika akiwa na umri wa miaka 37. Kuna mengi ya kujifunza kutoka kwake kwa wachezaji wote wa Man United.

Hag huenda akajenga kikosi cha vijana na kupandisha wachezaji wengi wachanga kwenye kikosi cha kwanza. Wachezaji hawa wanahitaji mshauri bora ambaye ni Ronaldo kwenye vyumba vya kubadilishia nguo.

Uundaji upya wa kikosi huwa mgumu kila wakati na timu zinahitaji watu mahiri katika vyumba vyao vya kubadilishia nguo ili kujadili nyakati ngumu kama hizi. Kwa upande wa Man United, wanamhitaji Ronaldo katika nyakati hizi.

**#2. Anaweza kuimarisha ulinzi, kiungo**

Kwa muda wote wa msimu huu na haswa katika wiki za hivi karibuni, Ronaldo amekuwa mfungaji bora wa kutegemewa kwa Man United. Amekuwa mtu wa kutisha katika nafasi tatu za mwisho kwa kikosi cha Ralf Rangnick.

Man United wanapaswa kuimarisha safu yao ya kiungo na ulinzi msimu huu wa joto. Usajili mpya kwenye safu ya kiungo unapaswa kupewa kipaumbele.

Wanaweza kutumia uboreshaji kwenye seti yao ya sasa ya mabeki wa pembeni pia. Iwapo watamtoa Ronaldo katika majira ya joto, basi Man United italazimika kutoa fedha ili kusajili mshambuliaji mpya pia.

Lakini kabla ya kufanya hivyo, wanatakiwa kuimarisha uti wa mgongo wa timu na kuwa na Ronaldo kwenye orodha kutawasaidia kuzingatia kuimarisha nafasi sahihi.

**#1. Anafaa kuwa nahodha badala ya Maguire**


Harry Maguire anapitia awamu ngumu sana katika kipindi chake cha uchezaji. Ameonekana kutojiamini na kuathiriwa sana na makosa msimu huu na hiyo ndiyo sababu mojawapo kwa nini hapaswi kubebeshwa tena unahodha.

Ni vigumu kwa timu kuangalia mchezaji ambaye hana kiwango kizuri na kupata msukumo kutoka kwake. Kwa ufupi, hiyo ndiyo hali ya mambo ndani ya Man United hivi sasa. Ingawa ni wazi kwamba United haijamvua Maguire unahodha wake ili tu kutomdhoofisha hadharani, ni hitaji la sasa.

Lakini ukichukua kitambaa hicho na kumpa Ronaldo, litakuwa chaguo la kimantiki. Ronaldo pia ni kiongozi sahihi ambaye anachukia kupoteza na kufanya vema katika kukusanya askari wake na kuongoza kwa mfano.

## ISIKUPITE

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Liverpool, Robbie Fowler, ndiye anayeshikilia rekodi ya kufunga mabao matatu 'hat-trick' ya haraka zaidi, ikiwa ni katika muda wa chini ya dakika tano kwenye Ligi Kuu England na timu aliyoifunga haikuwa iliyopo kwenye tishio la kushuka daraja, bali ni Arsenal. Fowler alipiga hat-trick hiyo ndani ya dakika nne na sekunde 33 kwenye mchezo uliopigwa Uwanja wa Anfield Agosti 28, mwaka 1994.



Extra Time

# WACHEZAJI AMBAO HAWAJAUTENDEA HAKI MSHAHARA WAO EPL



GREALISH

**LONDON,** England

LIGI Kuu England imekuwa nyumbani kwa baadhi ya wachezaji bora zaidi duniani kwa miaka mingi. Daima imekuwa ikiwavutia wanasoka kutokana na ushindani na umaarufu wake.

**Klabu za England zina nguvu sana kifedha na zinajitokeza linapokuja suala la kutoa mishahara ya kuvutia.**

Msimu wa 2021-22 umeshuhudia maonyesho ya kupendeza kwa wachezaji binafsi msimu huu. Ingawa hii ni kweli kwa wachezaji wengi, wengine hawajaweza kuvutia.

Wanasoka hawa wako kwenye malipo ya juu na wanajulikana sana. Wachezaji hawa wanapaswa kufanya vizuri zaidi kutokana na matarajio makubwa kutoka kwa klabu na mashabiki. Kwa maelezo hayo, tuwatazame wachezaji wa juu ambao wameshindwa kuhalalisha mishahara yao katika msimu huu wa Ligi Kuu England, haya sasa...

### #5. Saul Niguez (Chelsea)

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 27, alisajiliwa na Chelsea kwa mkopo katika dirisha la uhamisho wa majira ya joto kutoka Atletico Madrid. Kwa kuzingatia ubora wa ajabu alionao Niguez, alitarajiwa kuwa mchezaji muhimu wa 'The Blues' hao.

Kiungo huyo wa kati wa Hispania hapo awali alijitahidi kuingia kwenye kikosi cha kwanza. Alipopewa nafasi, Niguez alikuwa hana raha kwenye mpira kama kawaida akiwa na Atletico. Amekosa kujiamini.

Niguez kwa sasa anapokea mshahara wa pauni 198,269 kwa wiki akiwa na The Blues. Ikizingatiwa kuwa ameshindwa kuchangia bao hata moja kwenye ligi msimu huu, Mhispania huyo bila shaka anatakiwa kufanya vema zaidi.

### #4. Marcus Rashford (Manchester United)

Mshambuliaji huyu wa Manchester United, anajulikana sana ndani na nje ya uwanja. Marcus Rashford alikosekana kutokana na jeraha la bega mwanzoni mwa msimu wa huu wa 2021-22.

Tangu arejee, nyota huyo wa England hajaweza kumshawishi kocha wa muda, Ralf Rangnick kumwanzisha mara kwa mara. Hadi sasa, Rashford amefanikiwa kufunga mara nne na kusajili mabao mawili katika mechi 10 za Ligi Kuu.

Akiwa na mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki, mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 24, anatarajiwa kuwa na tija mbele ya lango. Ili kubadilisha kiwango chake, Rashford atalazimika kuboresha maamuzi yake katika nafasi ya tatu ya mwisho.

### #3. Timo Werner (Chelsea)

Timo Werner alikuwa mfungaji mabao wa kutisha alipoichezea RB Leipzig katika Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga. Katika misimu yake minne akiwa na klabu hiyo ya Ujerumani, alifunga mabao 78 na kusajili pasi za mabao 27.

Mshambuliaji huyo wa Ujerumani, alisajiliwa na Chelsea msimu uliopita na tangu wakati huo amepata ugumu kuwa mashine ya kupachika mabao alionao. Werner hadi sasa amefunga bao moja na kutoa asisti moja katika mechi 14 za Ligi Kuu msimu huu.

Kwa sasa anapokea mshahara wa pauni 272,000 kwa wiki akiwa na 'The Blues' hao na anatakiwa kuhalalisha hilo.

### #2. Jack Grealish (Manchester City)

Jack Grealish alikuwa mwanasoka ghali zaidi katika historia ya usajili kwenye Ligi England aliposajiliwa na Manchester City kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 100 msimu uliopita. Alikuwa akivutia sana akiwa Aston Villa kabla ya kuhamia kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu England.

Kwa wepesi wake, ustadi wa kusisimua akili na uwezo wa ubunifu, Grealish alitarajiwa kuwa na mchango mkubwa pale City. Hadi sasa, kiungo huyo wa kati hajaweza kufikia matarajio hayo.

"Sidhani kama ni siri kwa mtu yeyote kwamba ningependa kufunga zaidi na kusaidia zaidi msimu huu, lakini ninahisi kama nimekuwa nikicheza vizuri, hata wakati sijafunga au kusaidia," moja ya nukuu yake wakati akishutumiwa kutokuwa kwenye kiwango bora.

Licha ya kucheza mechi 19 kwenye ligi msimu huu, Grealish ana mabao mawili pekee na asisti mbili kwa jina lake. Akiwa na mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki, hata mashabiki wa City wangemtaka afanye vema zaidi.

### #1. Romelu Lukaku (Chelsea)

Mchezaji mwingine wa Chelsea kwenye orodha hii ni mshambuliaji nyota Romelu Lukaku. Mshambuliaji huyo wa Ubelgiji, alirejea kuichezea The Blues baada ya kuwa na wakati mzuri akiwa na Inter Milan katika Ligi Kuu Italia, Serie A, msimu uliopita. Aliweka rekodi ya usajili akiwa na Chelsea kwa pauni milioni 97.5.

Ni salama kusema kwamba kipindi cha pili cha Lukaku akiwa na Chelsea hakijawa sawa hadi sasa. Katika mechi zake 19 kwenye Ligi Kuu msimu huu, mshambuliaji huyo anayetumia mguu wa kushoto, amefanikiwa kufunga mara tano pekee. Mbelgiji huyo alifunga mabao 24 msimu uliopita akiwa na Inter katika mechi 36.


Lukaku kwa sasa anapokea mshahara wa pauni 325,000 kwa wiki. Kutokana na matarajio makubwa kutoka kwake na malipo yake, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, atalazimika kuboresha kiwango chake mbele ya lango.

## Nukuu


"Penalti ya Sadio ni jukumu langu kwa asilimia 50. Nilimwambia kipa anajua vizuri kile unachofanya kawaida, kwa hiyo fanya kinyume chake. Ni mara ngapi maishani mwangu ni bora kunyamaza! Lakini bado tulifanikiwa baada ya mchezo wa ajabu. Tunafanya kazi na kampuni ya sayansi ya neva (neruo11) ambao walisema wanaweza kufundisha mazoezi ya upigaji penalti. Taji hili ni lao pia," **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp akielezea kukosa penalti kwa Sadio Mane dhidi ya Chelsea juzi ni makosa yake.**



"Mashabiki wa Simba hawajawahi kuwa na hofu na kikosi chao, kama unavyoona leo (juzi dhidi ya Pamba FC) timu imecheza na kupata ushindi si kama zile penalti za dakika ya 98 na za 'naniino', lakini timu imecheza tutakutana na Yanga (nusu fainali FA), nategemea mechi itakuwa nzuri kama nao watakuwa wamejipanga kuja kucheza mpira," **Mwenyekiti wa Wanachama wa Klabu ya Simba, Murtaza Mangungu baada ya timu yao kushinda 4-0.**



"Unapofanikiwa maishani hata adui yako anageuka kuwa shabiki yako mkubwa," **Mashabiki wa PSG wakijibu picha ya Sargio Ramos 'akimtunza vizuri' Lionel Messi baada ya kuifungia PSG mabao mawili wakati ikishinda 4-0 dhidi ya Montpellier juzi. Ramos na Messi walikuwa wapinzani wakubwa wakati wakizichezea Real Madrid na Barcelona.**



# 'SAVES' TANO ZA MAANA LIGI KUU BARA UKINGONI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikielekea ukingoni, imeonekana kuwa ya moto, timu zikipigana vikumbo kwa kila hali kuhakikisha zinabaki kwa ajili ya msimu ujao.

**Kuna timu ambazo zinapigania nafasi ya tatu ili kucheza mechi za kimataifa msimu ujao kwa sababu Tanzania itapeleka timu nne, mbili ni zile zitakazoshika nafasi za juu ambazo zitacheza Ligi ya Mabingwa Afrika, moja ni bingwa wa Kombe la FA itakayocheza Kombe la Shirikisho Afrika, ikishirikiana na ile itakayomaliza nafasi ya tatu.**

Zipo timu mbili za Simba na Yanga zikifukuzana kusaka ubingwa.

Kutokana na hilo, wachezaji wamekuwa wakipambana sana ndani ya uwanja kuhakikisha timu zao zinapata kile ambacho zinapigania.

Moja ya nafasi zilizoonekana kuvutia kwenye wiki iliyoisha ni magolikipa, ambao wameonekana wengi kuwa kwenye viwango vya hali ya juu wakifanya 'saves' za maana kuziokoa timu zao zisiathirike.

Hata kama imetokea zimefungwa, lakini wamekuwa wakitimiza majukumu yao kama magolikipa.

Kwenye makala haya tunawaangalia makipa waliookoa michomo mikali ya maana wiki iliyopita kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, twende sasa...

**#1. Mohamed Makaka - Ruvu Shooting vs Simba**

Dakika ya pili tu ya mchezo Simba ilipata faulo nje ya eneo la hatari la Ruvu Shooting kwenye mechi ya Ligi Kuu iliyochezwa Mei 8 Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Alikuwa ni Pape Sakho aliyechukua jukumu la kupiga ambapo aliachia 'mashine' kali ambayo kama isingeguswa ingejaa wavuni, lakini kipa wa Ruvu Shooting, Mohamed Makaka, alikwenda juu na kuugonga 'konzi' mpira huo ukatoka nje kidogo juu ya lango na kuwa kona. Simba ilishinda mabao 4-1 kwenye mchezo huo.

**#2. Lameck Kanyonga - Mtibwa vs Mbeya City**

Ilikuwa ni dakika ya saba ya mchezo, ilipopatikana faulo umbali wa mita 35 kwenye mechi ya Ligi Kuu kati ya wenyeji Mtibwa Sugar dhidi ya Mbeya City, ilichezwa Uwanja wa Manungu Complex, Turiani, mkoani Morogoro, ikichezwa Mei 7.

Juma Shemvuni alitandika shuti kali ambalo kipa chipukizi wa Mtibwa Sugar, Lameck Kanyonga aliruka juu na kwenda kuugonga ngumi mpira ukatoka na kuwa kona. Ilikuwa moja kati ya 'save' bora kabisa kwenye Ligi Kuu na hadi mwisho, Mtibwa Sugar ilishinda bao 1-0, likiwekwa kambani na Hamisi Ndemla.

**#3. Ahmed Kadedi - Mbeya Kwanza vs Prisons**

Kipa wa Mbeya Kwanza, Ahmed Kadedi, aliiokoa timu yake kufungwa dakika ya 64 alipoucheza mpira akiwa ana kwa ana na straika wa Prisons, Jeremiah Juma. Aliingiziwa moja safi, akamuacha beki wa Mbeya Kwanza na kubaki na kipa. Akiwa na uhakika kuwa atafunga, alipiga shuti dhaifu pembeni, lakini kipa alijinyoosha na kuuokoa. Akanyanyuka na kuudaka tena. Kadedi alikuwa shujaa kwenye mechi hiyo kwa kuokoa michomo, mingi, lakini hiyo ilikuwa ndiyo hatari kubwa zaidi.

Mechi ilichezwa Mei 5 katika Uwanja wa Majimaji Songea, Mbeya Kwanza ikishinda bao 1-0, likiwekwa wavuni na Deo Mingwa kwa mkwaju wa penalti.

**#4. Ramadhani Chalamanda - Kagera Sugar vs Geita Gold**

Inawezekana kabisa straika wa Geita Gold, George Mpole angekuwa na mabao 13 mpaka sasa. Lakini amebaki na 12, kutokana na 'save' moja ya maana kutoka kwa kipa wa Kagera Sugar, Ramadhani Chamalanda.

Ilikuwa ni Mei 7 wakati Geita Gold ikishinda bao 1-0 lililopachikwa nyavuni na Mpole. Ilikuwa ni dakika ya 50 kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumbu, Geita, wakati Nashon Naftari alipoambaa na mpira winga ya kulia na kummegea pasi Mpole. Naye bila kutuliza aliiunga hivyo hivyo kwa shuti kali la juu lililoonekana linakwenda kutinga wavuni lakini kipa Chalamanda alisafiri na kuupangua mpira huo, hivyo kumnyima Mpole nafasi ya kuongeza mabao kwenye akaunti yake.

**#5. Kelvin Igendelezi -Polisi Tanzania vs Coastal Union**

Inawezekana kutokana na makosa ya mara kwa mara ya kipa Metacha Mnata, Polisi Tanzania wameamua kumchezesha kipa Kelvin Igendelezi na alionekana kwenye mechi dhidi ya Coastal Union katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga.

Pamoja na kufungwa bao 1-0 kwenye mechi hiyo, lakini kipa alifanya kazi ya ziada kupunguza mabao, moja ya 'save' bora ilikuwa ni dakika ya 61 alipopangua shuti kali akiwa ana kwa ana na Abdul Selemani ambaye ndiye pia aliyefunga mabao pekee kwa Coastal kwenye mechi hiyo.



Kipa wa Ruvu Shooting, Mohamed Makaka, mmoja wa makipa waliookoa michomo hatari kutoka kwa wachezaji wa timu pinzani kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. **PICHA: MAKTABA**

**JE, WAJUA?**

NCHI 12 za Afrika zitakazoingiza timu nne kwenye michuano ya Shirikisho la Soka Afrika msimu ujao; mbili Ligi ya Mabingwa na idadi kama hiyo Kombe la Shirikisho ni Morocco, Misri, Algeria, Tunisia, Afrika Kusini, DR Congo, Angola, Sudan, Libya, Guinea, Tanzania na Nigeria.



# Watakiwa kuheshimu mkataba kilimo mtama

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

WAKULIMA wa mtama wametakiwa kuheshimu mikataba waliyoingia na Kampuni ya Vinywaji ya Tanzania Breweries Limited (TBL) ya kununua zao hilo ili iwe na tija kwao.

Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Dodoma, Aziza Mumba, alitoa angalizo hilo mwishoni wa wiki alipokuwa akiwatembelea wakulima wenye mkataba hiyo wilayani Kongwa.

Mumba aliwahimiza wakulima hao kuzingatia usafi wa mazao yao wakati wa kuuza ili kujenga uaminifu wao kwenye mikataba na TBL.

"Ndugu zangu wakulima wa mtama mmepata bahati ya kumpata mnunuzi ambaye anawasaidia kuanzia mbegu bora za kupanda hadi kununua, hiyo ni bahati mnatakiwa kuendelea kujenga uaminifu kwa TBL,"alisema.

Alibainisha kuwa zao linastahili ukame hivyo wakulima wanatakiwa kuendelea kulima.

Alisema kutokana na hali hata wakulima waliolima mtama mwaka huu watapata mafanikio kuliko wale walionga'ang'ania kulima mahindi.

Pia alisema kilimo hicho kitawakomboa wakulima kutokana na uhakika wa kupata mazao ya kutosha na bei nzuri wanayopata wakulima kwenye vijijini vyao.

Naye Meneja Kilimo TBL, Joel Msechu, alisema wakulima 4,900 wa mtama waliingia mkataba wa kilimo hicho mkoani hapa kutoka wilaya za Mpwapwa, Chamwino, Kongwa, Chemba na Bahi.

Alisema kwa sasa ni mwaka wa tatu mfululizo wananunua mtama kwa ajili ya kuzalisha vinywaji kwenye viwanda vyao vilivyoko Arusha, Mbeya na Dar es Salaam.

Pia alisema TBL imewasaidia wakulima hao kwa kuingia nao mkataba wa kununua mazao yao na wamekuwa wakiwapatia mbegu bora kwa ajili ya zao hilo.

Aliongeza kuwa TBL imefanikiwa kuwaunganisha wakulima hao na taasisi za kifedha ili kupata mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya kununulia mbegu na pembejeo za kilimo.

Alisema pamoja na kununua mazao hayo kwa wakulima pia halmashauri husika zimekuwa zikinufaika kutokana na ushuru wa mazao unaolipwa na TBL.



Ofisa Kilimo wa Tanzania Breweries Limited (TBL), Joel Msechu (kushoto) na Ofisa Ugani, Harrison Mosha, wakikagua shamba la mfano la mtama la TBL lililoko Kibaigwa Wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma. Shamba hilo linatumika kuzalisha mbegu bora za mtama kwa ajili ya wakulima wa mkoa huo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Panya Road' waiamsha serikali Dodoma

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAMATI ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Dodoma imeweka mikakati ya kukabiliana na makundi ya kihalifu likiwamo la Panya Road ili kudhibiti matukio ya kujeruhi na kuiba mali za watu.

Hatua hiyo imekuja kutokoana na hivi karibuni mkoa wa Dar es Salaam kukabiliana na matukio ya makundi hayo ya kihalifu.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akifungua kikao cha kamati hiyo.

Alisema mkoa lazima kuweka mikakati ya kudhibiti matukio ambayo kwa sasa yamekuwa yakiripotiwa katika maeneo mbalimbali ambayo yamekuwa yakihatarisha usalama wa watu.

"Tumeona matukio ambayo yamekuwa yakitokea katika maeneo mengine yakihatarisha uvunjifu wa amani. Sasa tunasema tusisubiri hadi tupate matukio hapa Dodoma bali tujipange sasa. Tulishauriana katika kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa tuitishe kamati za wilaya ili kujadili suala la ulinzi na usalama wa mkoa wetu.

"Ukiona leo Dar es Salaam wanahangaika na Panya Road lazima kuanza kujiandaa katika maeneo yetu namna ya kukabiliana na watu wa aina hiyo bila kusubiri yatokee ndipo mikakati ianze kuwekwa," alisema.

"Tumeanza kushuhudia matukio yakitokea katika maeneo mbalimbali yakihatarisha maisha na sisi Dodoma hatuwezi kusubiri yatokee ndipo tuanze kujiimarisha kwa sababu kuna msemo unasema mwenzako akinyolewa zako tia maji.

Baada ya kikao hiki, nitafanya kikao na bodaboda na bajaji kwa sababu watu wengi hawaamini vyombo vya usafiri hivi kutokana na kutumika kufanya uhalifu na kuharibu taswira yao katika jamii," alisema.

Mkuu huyo wa mkoa alitaja mikakati waliyokubaliana katika kukabiliana na uhalifu kuwa ni kuhakikisha Jeshi la Polisi linatekeleza wajibu wake kwa weledi na ushirikishaji wa wananchi katika kukabiliana na vitendo vya kihalifu.

"Kila mmoja katika eneo lake aonyeshe ujuzi na umahiri wa taaluma yake katika kukabiliana na uhalifu ndiyo maana kazi hii haiwezi kufanywa na watu wengine zaidi ya polisi. Lazima kuweka mikakati kuhakikisha kila taarifa ya uhalifu ipo kiganjani mwenu. Nataka mpate moyo wa kunguru maisha ya watu ili watu wajue Dodoma ni salama," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martine Otieno, alisema serikali za mitaa ni kiungo muhimu katika kuziunganisha shughuli za polisi jamii na wananchi katika kuimarisha ulinzi na usalama wa eneo husika.

# BRELA yahimiza urasimishaji biashara

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAKALA wa Usajili Majina ya Biashara na Leseni (BRELA), umewataka Watanzania kurasimisha kampuni na biashara zao ili kupata fursa za mikopo, zabuni na mitaji kutoka kwa wawekezaji wa nje.

Ofisa Usajili Msimamizi wa Kanda ya Dodoma, Gabriel Girangay, alitoa wito huo juzi alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya ufunguzi wa mkutano mkuu wa mwaka wa Bodi ya Usajili Makandarasi (CRB).

Girangay alisema urasimishaji wa kampuni, biashara na viwanda vidogo ni jambo la muhimu ili wamiliki wapate mikopo kutoka taasisi za fedha pamoja na zabuni mbalimbali.

"Ukirasimisha biashara yako, ziko faida nyingi sana kama vile kupata mikopo, kupata zabuni mbalimbali lakini pia kupata mitaji kutoka kwa wawekezaji kutoka nje ambao wanaweza kuwekeza katika kampuni za wazawa. Kazi ya BRELA ni kutoa elimu, kusajili kampuni na biashara, kutoa leseni ya biashara kundi A, kwa viwanda vidogo na kutoa leseni," alisema.

Pia alisema wananchi hawatakiwi kutishwa na maneno ya watu ambao wamekuwa wakidai kuwa wakala huo umekuwa na urasimu katika utekelezaji wa majukumu yake.

Kadhalika, alisema hivi sasa wanao mkakati wa kuhakikisha wanawafikia wananchi wote katika kila eneo la Tanzania.

Alisema elimu wanayotoa ni pamoja na namna ya kusajili kampuni, biashara viwanda vidogo na vya kati, kutoa leseni na kutatua kero mbalimbali zinazowakabili.





# Mbeya yaelemewa watoto wa mitaani

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

HALMASHAURI ya Jiji la Mbeya inakabiliwa na ongezeko la watoto wa mitaani na wanaoishi katika mazingira magumu kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo wazazi kufariki dunia, kukimbia manyanyaso kutoka kwenye familia na mifarakano ya wazazi.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Jiji hilo, Eva John, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati idara yake iliposhirikiana na Jeshi la Polisi kuwakamata watoto 39 wa mitaani waliokuwa wanaishi kwenye maeneo mbalimbali likiwamo soko la Sido.

Alisema idadi ya watoto wa mitaani katika jiji hilo ni kubwa na wamekuwa wakikamatwa mara kwa mara na kuunganishwa na familia zao, lakini baadhi yao wanatoroka tena na kurejea mitaani kutokana na matatizo mbalimbali.

Kwa mujibu wa John, baadhi ya watoto hao wamekuwa wakijiingiza kwenye matukio ya uhalifu kutokana na makundi wanayokutana nayo mitaani wanakoishi na kwamba wengine wanaingia kwenye makundi ya wizi kama inavyotokea kwenye mikoa mingine kama Dar es Salaam.

"Hawa watoto tunachokifanya baada ya kuwakamata ni kufanya taratibu za kuwaunganisha na familia zao. Lakini kiufupi ni kwamba tatizo la watoto wa mitaani katika jiji letu ni kubwa, ofisini kwangu nina takwimu za watoto hawa," alisema John. Alisema kutokana na tatizo hilo, ofisi yake imeanza kuwekeza nguvu kubwa kwenye kutoa elimu kwa jamii kuhusu namna ya kuishi na watoto bila kuwakwaza watoto na kusababisha wakimbilie mitaani.

Baadhi ya watoto, alisema wanatoroka kwenye familia zao kutokana na kukwepa majukumu yao ya kawaida ikiwamo kusaidia kazi za nyumbani na wengine wanakuwa wanakwepa kwenda shuleni.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alisema walifanya msako katika maeneo mbalimbali ya jiji na kuwakamata watoto hao wakiwa wanaishi kwenye mazingira hatarishi.

Alisema watoto hao walikuwa wanaishi kwenye mapagala na maeneo ya maduka ya Sido, Mwanjelwa na Mafiati na kwamba baadhi ni wahalifu na wamewahi kushtakiwa kwa makosa mbalimbali.

Matei alisema watoto waliokamatwa wana umri wa kati ya miaka 10 na 16 na kwamba hakuna mwenye umri zaidi ya miaka hiyo na hivyo akawataka wazazi kuwalea watoto wao katika malezi bora.

"Mmoja wa watoto hawa alishtakiwa kwa kosa la kukata nyaya za umeme shuleni na alipoachiwa alirejeshwa nyumbani kwao alitoroka tena na kwenda kuishi mitaani na aliacha shule, sasa tunawashirikiana na ustawi wa jamii kuwaunganisha na familia zao," alisema Kamanda Matei.

Aliwataka wazazi kuepuka kuwafanyia ukatili watoto kwa maelezo kuwa vitendo hivyo ndivyo vinavyosababisha watoto wa mitaani kuongezeka huku akisisitiza kwamba maeneo hayo watoto wanajifunza tabia mbaya.

Alisema watoto waliokamatwa karibia wote wana umri ambao walitakiwa wawe wanasoma shule za msingi ama sekondari lakini wote hawasomi.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda akiangalia namna uchapishaji wa vitabu vya uono hafifu ukifanyika baada ya kufanya ziara ya kutembelea Kiwanda cha uchapaji wa vitabu cha Press A na Press B jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waathirika mafuriko wapatiwa misaada

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WANANCHI waliokumbwa na mafuriko wilayani Kyela kati ya Aprili 27 na 29, mwaka huu, wameanza kupata misaada kutoka kwa wadau mbalimbali nchini ikiwamo serikali kuu.

Mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alikabidhi zaidi ya magodoro 150, mahema 15, mablanketi, mashuka, mafuta ya kupikia, chakula na sukari kwa baadhi ya waathirika na akakabidhi kwa uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kwa ajili ya kuwagawia wahusika.

Baadhi ya vitu hivyo ambavyo wananchi hao walipatiwa vilitoka katika Ofisi ya Waziri Mkuu Kitengo cha Maafa, vingine vilitolewa na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) ambavyo ni mafuta ya kupikia na sukari.

Homera alitoa siku mbili kwa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela kuhakikisha inagawa vitu hivyo kwa waathirika wa mafuriko hayo bila kubagua kwa maelezo kuwa msaada huo ni kwa ajili ya wahanga wa mafuriko wote. Alisema haitakiwi kuwe na ubaguzi wa aina yoyote wakati wa kugawa msaada huo huku akiwataka wananchi hao kutumia vifaa hivyo kwa matumizi yaliyolengwa.

"Hakikisheni mnasimamia vitu hivi viende kwa wahusika na kisipotee kitu chochote, lakini sitegemei kirudishwe kitu chochote kwa sababu wamehesabiwa waathirika na wanajulikana kutokana na tathmini iliyofanywa," alisema Homera.

Aliwaomba wadau mbalimbali waendelee kuwasaidia wananchi hao kwa maelezo kuwa mafuriko hayo yaliwasababishi madhara makubwa kwa wananchi hao.

Meneja wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Matrida Kunenge, alisema mamlaka hiyo ilitoa kilo 2,800 za sukari na lita 450 za mafuta ya kupikia ambavyo waliagizwa na Kamishna Mkuu wa TRA kuvitoa kwa waathirika baada ya kupata taarifa. Alisema vitu hivyo ni vile ambavyo walivikamata kwenye operesheni mbalimbali za kukamata biashara za magendo kwenye maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

"Tuliagizwa na Kamishna tutoe vitu hivi kwa wenzetu hawa wahanga (waathirika). Tumevitoa vitu hivi kutokana na shughuli zetu ambazo tumekuwa tukizifanya," alisema Kunenge. Mkurugenzi wa Idara ya Menejimenti ya Maafa kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Michael Mumanga, alisema Kyela ni miongoni mwa wilaya saba nchini ambazo zimekuwa zikikumbwa na maafa ya mara kwa mara.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Magereza Ismail Mlawa, aliishukuru serikali kwa kutoa msaada huo akisema wananchi walipata shida kubwa baada ya mafuriko hayo kutokea.

Alisema mafuriko hayo yaliathiri zaidi ya watu 1,500 na zaidi ya nyumba 400 ziliathirika kwa baadhi kubomoka na zingine kuharibika huku chakula kikisombwa na mafuriko hayo kwenye vijiji 41 vya wilaya hiyo.

Wilaya ya Kyela imekuwa ikikumbwa na mafuriko kila mwaka kutokana na mvua ambayo imekuwa ikinyesha katika wilaya za Mbozi, Momba na Ileje mkoani Songwe pamoja na Wilaya za Mbeya na Rungwe mkoani Mbeya.

Mvua hiyo imekuwa ikisababisha kujaa kwa mito mbalimbali ikiwamo Mto Songwe, Mto Kiwira na Mto Mbaka ambayo ndiyo imekuwa ikileta madhara zaidi kwa wananchi.

## Taasisi ya Tulia yasaidia polisi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Tulia Trust inayomilikiwa na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, imeanza kuboresha miundombinu ya vituo vya polisi katika maeneo mbalimbali ya mkoa wa Mbeya kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji kazi.

Taasisi hiyo ilianza kuboresha miundombinu hiyo kwa kuanzia katika kituo kikuu cha polisi cha wilaya ya Kyela ambako ilikabidhi vifaa vya kuunganishia maji yakiwamo mabomba, mota ya kuvutia maji na nyaya za umeme.

Pia ilikabidhi mbao 60 na mabati 32 kwa ajili ya kuezeka kituo kidogo cha polisi kilichoko katika eneo la Stendi Kuu ya Mabasi ya Mkoa wa Mbeya ambacho kimekuwa kikivuja wakati wa mvua kutokana na kuwa na mabati chakavu.

Akikabidhi vifaa hivyo, Meneja wa Tulia Trust, Jacqurene Boaz, alisema taasisi hiyo ilipokea maombi mbalimbali kutoka kwenye vituo hivyo kwa ajili ya kuboresha miundombinu na kwamba ndio maana waliamua kukabidhi.

"Kila kituo walituletea maombi tofauti, Kyela waliomba kusaidiwa miundombinu ya maji kutokana na kuwa na shida ya huduma hiyo na ndiyo maana tumewapatia hivyo, lakini hapa mjini waliomba mabati na mbao," alisema Boaz.

Alisema wanatoa vifaa hivyo vya kusaidia jamii kutokana na malengo ya taasisi hiyo kuwa ni kusaidia makundi mbalimbali ya jamii vikiwamo vyombo vya ulinzi na usalama.

Akipokea vifaa hivyo kwa niaba ya Jeshi la Polisi, Mkuu wa Kituo Kidogo cha Polisi cha Stendi Kuu, Daiman Kagete, alisema msaada waliopata utawasaidia kupunguza tatizo la uchakavu wa kituo hicho ambacho alisema kilikuwa kinavuja wakati wa mvua.






Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar, Simai Mohammed Said, akizungumza katika kongamano la wadau wa utalii lililoandaliwa na Benki ya NMB visiwani humo mwishoni mwa wiki. Kulia ni Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya NMB, Benedicto Baragomwa na Meneja wa Kanda ya Dar es Salaam wa benki hiyo, Donatus Richard, wakimsikiliza. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB yakutana na wadau wa utalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BENKI ya NMB imekutana na wadau wa utalii Zanzibar ili kusukuma mbele sekta hiyo baada ya Rias Samia Suluhu Hassan kuzindua filamu ya Royal Tour.

Akizungumza katika uzinduzi wa kongamano la mtandao wa utalii lilofanyika katika hoteli ya Madinatulbahar mjini Zanzibar, Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, alisema benki hiyo imetenga Sh. bilioni 100 kwa ajili ya sekta ya utalii.

Alisema Zanzibar ina fursa nyingi na wakiwa wadau wana jukumu la kuhakikisha sekta ya utalii inarudi na kuongeza ufanisi baada ya janga la corona liloikumba dunia.

Richard alisema fedha hizo, Sh. bilioni 100 ni kwa ajili ya kutoa mikopo mbalimbali kwa sekta ya utalii ikiwamo kuwapatia watembeza watalii kwa ajili ya kusaidia sekta ya utalii Zanzibar.

Alisema watahakikisha wanatoa elimu jinsi ya kuzitumia fedha watakazokopeshwa kwa ajili ya shughuli za utalii ili fedha watakazopewa kuzitumia kwa lengo lililokusudiwa.

"Hii ni fursa kwa hivyo nitowe wito kuchangamkia fursa hii ili kunufaika na huduma zinazotolewa na NMB," alisema.

Alisema sekta ya utalii ni muhimu sana na ni kichocheo kikubwa cha uchumi wa bluu, hivyo wataimarisha mfumo wa kuwapokea watalii wanaoingia Zanzibar kwa njia ya mtandao.

Pia aliwataka wadau wa utalii kujiandaa kuwapokea na kuwahudumia watalii wengi ambao wanatarajiwa kuwasili Tanzania kutokana na filamu ya Royal Tour iliyozinduliwa hivi karibuni na Rais Samia.

Akizindua uzinduzi huo, Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Muhammed Said, alisema sekta ya utalii imepita katika kipindi kigumu cha mlipuko wa UVIKO-19 yaliyodhoofisha utalii duniani kote, hivyo fedha hizo zitachochea kurudi kwa wadau wa utalii na kuibua fursa mpya.

Alishauri NMB kuandaa mafunzo maalum ya matumizi ya simu janja kwa watakaochukua mkopo huo ili kuibua fursa mpya ndani na nje ya nchi.

"NMB mnatuonyesha njia na mko karibu na wananchi katika kusogeza huduma zenu hivyo niwapongeze sana kwa jitihada zenu hizo," alisema.

Mwenyekiti wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Rahim Baloo, ameitaka NMB kuweka masharti nafuu kwa wadau wa utalii na kuwajengea uwezo ili kuhimili ushindani wa soko.

Pia aliwataka wadau wa utalii kuzitumia fursa zilizopo katika sekta hiyo ikiwamo kuwatumia watu mashuhuri wanaofika Zanzibar ili kupata soko katika sekta ya utalii.

# Waziri aeleza mafanikio ya maridhiano

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu wa Shughuli za Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, amesema maridhiano ya kisiasa Zanzibar yamefungua milango ya maelewano na wananchi kuzika tofauti zao za kisiasa za chuki na uhasama.

Aliyasema hayo juzi mjini Zanzibar wakati akizinduwa mradi wa 'Tujenge Maridhiano' ambao unatekelezwa na Taasisi ya Search for Common Ground chini ya ufadhili wa ubalozi wa Marekani.

Hamza alisema maridhiano hayo ndiyo kipaumbele cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuyafikia maelewano ya kweli na kuzika tofauti za siasa za chuki na uhasama.

Alisema mafanikio ya maridhiano ya kisiasa yataendelea kudumu iwapo wanasiasa wataachana na kauli za chuki na uchochezi katika majukwaa yenye mwelekeao wa kufarakana.

Waziri Hamza aliwataka wanasiasa kutumia nafasi zao kwa kuikosoa serikali kwa utaratibu unaofahamika lakini si kuwahamasisha wananchi kujenga chuki na uhasama kwa viongozi wao.

Alizipongeza asasi za kiraia nchini kwa kazi kubwa ya kutekeleza miradi ya kuhamasisha amani na utulivu na idumu kipindi chote kabla na baada ya uchaguzi mkuu.

"Nimefurahishwa na mchango mkubwa wa asasi za kiraia ambazo zimekuwa zikitafuta miradi yenye kuelimisha umuhimu wa amani na utulivu wa kisiasa. Wimbo wetu ni amani na maridhiano ya utulivu," alisema Hamza.

Naye Mwakilishi wa Ubalozi wa Marekani nchini, Kristine Mencer, alisema amefurahishwa kazi nzuri inayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan ya kuonana na wanasiasa wakiwamo wapinzani kuzungumzia mustakabali wa nchi katika mwelekeo wa kisiasa na kukuza demokrasia.

Alisema kitendo cha kuunda kikosi kazi kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi changamoto za kisiasa na demokrasia ni matumaini mapya ya kuimarika kwa siasa za vyama vingi.

Pia aliipongeza Serikali ya Zanzibar kwa kuendelea kuimarisha maridhiano ya kisiasa ambayo yameimarisha utulivu wa kisiasa na kufungua milango kwa wawekezaji zaidi nchini.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Search for Common Ground, Hussein Faraji Sengu, alisema mradi huo ni wa mwaka mmoja ambao lengo lake ni kuhimiza maridhiano ya kisiasa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwamo viongozi wa vyama vya siasa na viongozi wa dini kuhusu ujenzi wa demokrasia na amani.

# Hemed awa mbogo ujenzi wa masoko

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ametoa muda maalum kuanza kwa ujenzi wa masoko ya Chuini na Jumbi yalioko Unguja ambayo yamekaa kwa muda mrefu bila kuanza kwa ujenzi.

Hemed alitoa muda huo juzi katika ziara ya kukagua ujenzi wa miradi ya masoko ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema hajafurahishwa na hatua iliyofikiwa katika soko la Chuini na kusema taarifa za ujenzi huo zilizotolewa na mwekezaji na mkandarasi si za kuridhisha, hivyo kuuagiza uongozi wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kukaa na mwekezaji ndani ya wiki mbili na hatimaye ujenzi huo uanze.

Kuhusu ujenzi wa soko la Jumbi, Hemed alitoa mwezi mmoja kwa mkandarasi kuanza kazi katika soko hilo.

Pia aliitaka Wizara ya Tawala za Mikoa kufanye ukaguzi yakinifu juu ya wawekezaji hao na utakapotokea ugumu wa aina yoyote, kutoa taarifa serikali kuu ili kutafuta njia mbadala ya kupata fedha za ujenzi wa masoko hayo.

Makamu wa Pili huyo alisema uwepo wa masoko hayo utasaidia kustawisha hali za wananchi na wafanyabiashara kuwa na mazingira mazuri ya kufanyia kazi na kukuza kipato chao na serikali kukusanya mapato kwa kukuza uchumi wa nchi.

Alitoa onyo kwa baadhi ya viongozi kuacha tabia ya kuwaunga mkono wawekezaji wababaishaji ambao wameingia mkataba na serikali kwa kuonyesha nia njema badala yake wamegeuka na kuitia doa serikali. Kutokana na kuwapo kwa watu wa aina hiyo, alionya kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Muhamed, alisema wizara yake kupitia serikali ya wilaya na ya mkoa, watasimamia na kufuatilia ujenzi huo.

Masoud alisema wako wawekezaji wanaharibu dhamira ya serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi kuonya kuwa wizara haitowavumilia.

HABARI KIMATAIFA

# Ukraine yaanza kuurejesha mji wa Izium

**KYIV,** Ukraine

VIKOSI vya Ukraine vimeanza operesheni ya kuurejesha mikononi mwao mji wa mashariki wa Izium.

Hatua hiyo ni mkakati maalum wa mapambano ya kuwarejesha nyuma wanajeshi wa Russia katika eneo la Donbas

Kwa sasa, vikosi vya Russia vinaonekana kuelekeza nguvu zake zaidi kwenye mkoa huo wa Donbas wenye utajiri wa viwanda katika kile kinachoelezwa awamu ya pili ya uvamizi wake iliyotangazwa Aprili 19, mwaka huu, baada ya kushindwa kuuchukuwa mji mkuu, Kyiv.

Lakini vikosi vya Ukraine vimekuwa vikiyarejesha mikononi mwake maeneo ya kaskazini mashariki na kuwafurusha wanajeshi wa Russia kutoka mji wa pili kwa ukubwa wa Kharkiv.

**Mbali ya kupoteza idadi kubwa ya wanajeshi na vifaa vya kijeshi, Russia pia imeathirika vibaya kwa vikwazo vya kiuchumi.**

Kwa kuendelea kuweka shinikizo lake kwenye mji wa Izium na kukata njia ya usafirishaji vifaa na bidhaa vya Russia, kutafanya iwe shida kwa wanajeshi kuvizunguka vikosi vya Ukraine kutokea upande wa mbele wa jimbo la Donbas.

### URUSI YADAI KUUA WANAJESHI 100

Hata hivyo, Wizara ya Ulinzi ya Russia ilisema vikosi vyake viliyashambulia maeneo kadhaa ya kijeshi ya Ukraine, yakiwamo ya Donbas, na kuwaua wanajeshi 100.

Hata hivyo, taarifa hiyo haikuweza kuthibitishwa na vyanzo huru vya habari.

Rais Volodymyr Zelensky wa Ukraine, alisema kwamba hali katika eneo la Donbas bado ni ngumu, akiongeza kwamba vikosi vya Russia bado vinajaribu kujipatia aina fulani ya ushindi licha ya kukabiliwa na upinzani mkali.

### UUNGAJI MKONO ZAIDI WA KIMATAIFA

Katika ishara nyingine ya mshikamano wa kimataifa, maseneta wa Chama cha Republican cha Marekani, wamefanya ziara ya kushtukiza mjini Kyiv.

Rais Zelensky alisena ujumbe huo wa Republican ulijadili hatua zaidi za kuongeza vikwazo dhidi ya Russia.

Wachambuzi wa Kimagharibi walidai kuwa Rais Vladimir Putin wa Russia alishindwa kukisia upinzani mkali wa kijeshi wa Ukraine na hatua kali za dunia dhidi yake, wakati alipoamuru uvamizi wa tarehe 24 Februari.

Mbali ya kupoteza idadi kubwa ya wanajeshi na vifaa vya kijeshi, Russia pia imeathirika vibaya kwa vikwazo vya kiuchumi.

Kundi la mataifa saba tajiri yanayoongoza uchumi wa Magharibi liliahidi kwenye taarifa yao ya pamoja siku ya Jumamosi kwamba wangeliendelea kukuongeza shinikizo la kiuchumi na kisiasa dhidi ya Russia. **DW**



Moshi ukifuka katika kituo cha kijeshi eneo la Lviv nchini Ukraine baada ya kushambuliwa na makombora ya Russia jana. **PICHA: BBC**

## Palestina yaunga mkono uchunguzi kifo cha mwandishi wa Al Jazeera

**Jerusalem,** Palestina

MAMLAKA ya Palestina imesema itaukaribisha msaada wa kimataifa katika uchunguzi wa kifo cha mwandishi wa habari wa Al Jazeera, Shareen Abu Akeb (pichani chini).

Hata hivyo, Israel ilisema itachunguza kuzuka kwa vurugu katika mazishi yake.

Polisi wa Israel waliuvamia na kuushambulia msafara wa waombolezaji wa Kipalestina, kwenye eneo la Mji Mkongwe waliokuwa wamebeba jeneza la mwandishi huyo, tukio ambalo limesababisha jumuiya ya kimataifa kulilaani.

Vurugu hizo ziliongeza hasira kwa Wapalestina baada ya mauaji ya Shereen, ambayo yametishia kuchochea mivutano ambayo imekuwa ikiongezeka tangu Machi mwaka huu

Waziri wa Usalama wa Ndani wa Israel, Omer Barlev, alisema kuwa yeye na kamishna wa polisi wamekwishateua jopo la kufanya uchunguzi wa kina wa kile kilichotokea wakati wa mazishi na kwamba matokeo ya uchunguzi huo yatatolewa katika siku zijazo.

Mamlaka ya Palestina imekielezea kifo cha mwandishi huyo wa habari, ambaye alikuwa akiripoti uvamizi wa Israel katika eneo la Ukingo wa Magharibi linalokaliwa kwa mabavu kama tukio la mauaji la vikosi vya Israel. **DW**



## 10 wauawa kwa ubaguzi wa rangi Marekani

**NEW YORK,** Marekani

MWANAUME mmoja mzungu amewapiga risasi watu 10 katika kitongoji cha watu weusi jimbo la New York katika kile mamlaka inaita shambulizi lililochochewa na ubaguzi wa rangi.

Mwanaume huyo, mwenye miaka 18 aliyetajwa kwa jina la Payton Gendron katika nyaraka za mahakama, alikamatwa baada ya majibizano ya risasi katika eneo la tukio hilo kwenye duka katika jiji la Buffalo.

Tukio hilo lilitokea juzi mchana wakati mshukiwa huyo aipoingia katika duka hilo kabla ya kufyatua risasi kiholela na kuirusha mtandaoni.

Rais wa Marekani, Joe Biden, alilaani kile alichokiita kitendo cha kuchukiza.

"Tunachunguza tukio hili kama uhalifu wa chuki na kesi ya itikadi kali za kikabila," alisema Stephen Belongia, kutoka ofisi ya FBI ya Buffalo.

Aliongeza kuwa kuna ushahidi wa uwepo wa uadui wa rangi.

Habari za CBS ziliripoti kwamba mshambuliaji alipiga kelele za kibaguzi wakati wa ufyatuaji risasi na kusema kuwa alikuwa na maneno ya kikabila yaliyoandikwa kwenye silaha yake.

Pia inaonekana alichapisha taarifa mtandaoni iliyojumuisha lugha na mawazo ya ubaguzi wa rangi. Mshukiwa anaaminika kuwa aliendesha gari kwa takriban maili 200 kufika eneo lenye watu weusi wengi jijini humo.

Watu 13 walipigwa risasi kwa jumla na wengi waathiriwa walikuwa weusi, Kamishna wa Polisi wa Buffalo Joseph Gramaglia alisema.

Alisema alitoka kwenye gari lake akiwa na silaha nyingi, ikiwamo vifaa vya mbinu mbalimbali.

"Alikuwa amevaa kofia ya chuma. Alikuwa na kamera ambayo alikuwa akirusha moja kwa moja alichokuwa akifanya," Gramaglia aliwaambia wanahabari.

Alisema mtuhumiwa alisalimisha silaha yake baada ya hali ya wasiwasi na kupelekwa mahabusu. Baadaye alifikishwa mahakamani akishtakiwa kwa mauaji ya kiwango cha kwanza.

Waathiriwa watatu waliojeruhiwa - ambao wote walifanya kazi katika duka hilo hawajapata majeraha makubwa

Ofisa wa polisi aliyestaafu ambaye alikuwa akifanya kazi kama mlinzi alijaribu kumpiga risasi mshukiwa lakini alikuwa miongoni mwa waliouawa, polisi walisema. **BBC**

# DJUMA, LUSAJO VINARA WA 'ASSIST' LIGI KUU TANZANIA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Fiston Mayele wa Yanga na George Mpole wa Geita Gold wakiongoza orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara wakiwa na mabao 12 kila mmoja, straika aliyewahi kuongoza kwa magoli mwanzoni, Reliants Lusajo wa Namungo, sasa amekuwa kinara wa kutoa pasi za mabao.

Lusajo ambaye anashika nafasi ya pili kwenye orodha ya wafunga mabao mengi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa akiwa nayo 10 ametoa pasi nne za mabao, hivyo kuhusika katika jumla ya mabao 14 mpaka sasa.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, straika huyo anaongoza kundi la wachezaji wenye 'asisst' nyingi kwenye Ligi Kuu, akiwa sawa na Djuma Shaaban wa Yanga.

**Mbali na beki hiyo wa kulia wa vinara wa Ligi Kuu, kiungo wa Azam FC, Tepsi Evance pia ana idadi hiyo ya 'assist', yupo pia Pius Buswita wa Ruvu Shooting, Chiristian Zigah wa Biashara United na Aboubakar Ngalema wa Dodoma Jiji.**

Kwa upande wa mbio za ufungaji bora, straika wa Azam FC, Rodgers na Denis Kibu wa Simba wameonekana kuwa ingizo jipya kwenye kinyang'anyiro hicho.

Kwa mechi za karibuni, wameonekana kufunga mabao mfululizo kwenye mechi za Ligi Kuu, hivyo kutishia nafasi za watu wengine ambao kwa muda mrefu wamekuwa hapo na hawapandi juu, lakini kwa vinara wenyewe.

Kola amefikisha mabao saba mpaka sasa, huku Kibu akiwa na mabao sita.

Meddie Kagere ameendelea na mabao yake saba kwa muda mrefu, Saido Ntibazonkiza wa Yanga naye akiwa na mabao sita kwa kipindi kirefu sasa.

## CHA PILI HICHO...




Mshambuliaji wa Simba, Kibu Denis, akiifungia timu yake bao la pili kwa kichwa wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Pamba FC kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi. **PICHA: SIMBA**

# Mo apongeza ubingwa Simba Queens

**Na Saada Akida**

MWEKEZAJI na Rais wa Heshima wa Simba, Mohammed "Mo" Dewji, amekipongeza kikosi cha timu ya Wanawake cha Simba, Simba Queens, kwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake nchini mara tatu mfululizo.

Simba Queens juzi walitawazwa kuwa mabingwa wa ligi hiyo baada ya ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mlandizi Queens, matokeo ambayo yaliwafanya 'Malkia wa Msimbazi' hao kufikisha pointi 57 ambazo haziwezi kufikia na timu yoyote katika ligi hiyo msimu huu.

Kupitia ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Instagram, billionea huyo kijana Afrika, Mo Dewji, aliandika: "Hongera kwa timu yetu ya Simba Queens kwa kutwaa ubingwa wa tatu mfululizo wa Ligu Kuu ya Wanawake, niwapongeze benchi la ufundi na wachezaji kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya kutuletea heshima Msimbazi na sisi tunafurahia mafanikio yenu."

Wakati Mo akitoa pongezi hizo, Nahodha wa Simba Queens, Fatma Issa 'Fetty Densa', amefichua siri ya kutwaa ubingwa wa huo kwa mara ya tatu mfululizo kuwa kumetokana na kujituma na kufuata vema maelekezo ya benchi la ufundi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Sebastian Nkoma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Fetty alisema haikuwa kazi rahisi kutetea taji hili kwa kutokana na upinzani mkali uliopo katika ligi hiyo kwa sasa, ila kujituma na kufuata maelekezo ya benchi la ufundi ndio siri kubwa ya mafanikio hayo.

Alisema pamoja na kupata mafunzo mazuri kutoka benchi la ufundi, lakini mwalimu wao amekuwa akiwasisitizi kujituma uwanjani ili kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kutetea ubingwa jambo ambalo wamelikamilisha.

"Ni jambo la kumshukuru Mungu kwa kufanikiwa kutwaa ubingwa wa ligi mara tatu mfululizo, haikuwa kazi rahisi, lakini kujituma na kufuata maelekezo ya mwalimu ndio siri ya mafanikio haya," alisema Fetty Densa.

# BMT yatoa rai uchaguzi TPBRC

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), limewataka viongozi wapya wa Kamisheni ya Ngumi za Kulipwa nchini (TPBRC), kuhakikisha hadi kufikia uchaguzi mkuu wa 2023, wanakuwa na nusu ya wanachama kikatiba katika mikoa yote nchini.

Kauli hiyo ilitolewa juzi katika uchaguzi mdogo wa TPBRC, uliofanyika Dar es Salaam, kujaza nafasi ya rais, mweka hazina na wajumbe wawili, zilizokuwa wazi ili kukamilisha kamati ya utendaji kwa mujibu wa katiba ya kamisheni hiyo.

Katika uchaguzi huo, Chauremb Palasa (pichani chini) bondia wa zamani na mwamuzi wa mchezo wa ngumi za kulipwa nchini, alishinda nafasi ya rais kwa kupata kura kumi (10) akimshinda Meja Bakari Songoro aliyepata kura tisa (9) na Michael Chatta akiambulia kura sufuri.

Kwa upande wa mweka hazina, Elias Mlundwa aliibuka kidedea kwa kupata kura 17 za ndiyo na kura mbili za hapana za wapiga kura19 waliopiga kura hizo katika uchaguzi huo.

Nafasi ya wajumbe Ibrahim Kamwe ameshinda kura 19 na Amos Mwamakula akipata 17 na Bakari Khatibu akiambulia kura nane pekee.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Michezo Mkuu wa BMT, Allen Alex, alisema viongozi hao wa TPBRC wanatakiwa kuhakikisha wanachama wanajisali kwa mujibu wa sheria za BMT pamoja na kushughulikia migogoro ndani ya kamisheni hiyo.

Alisema kamisheni hiyo imekuwa inaongoza kwa migogoro ya ndani kwa ndani hali ambayo wanatakiwa kufanyia kazi kuhakikisha suala hilo linamalizika ili kusimamia madhubuti mchezo huo.

"Viongozi wanatakiwa kuhakikisha hadi uchaguzi mkuu wa mwaka 2023, kamisheni inafanikiwa kuongeza nusu ya wanachama wa kikatiba kutoka mikoani," alisema Allen.



## ZISIKUPITE

### JESUS KUTUA ARSENAL

ARSENAL inaandaa ofa ya ufunguzi ya kumnunua mshambuliaji wa Manchester City, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 25. City wanataka kati ya euro milioni 50 na euro milioni 60 kwa ajili ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil. ***(Fabrizio Romano)***

### KANTE ATAKIWA UNITED

KOCHA ajaye wa Manchester United, Erik ten Hag anamlenga kiungo wa kati wa Ufaransa na Chelsea, N'Golo Kante mwenye umri wa miaka 31, huku akitarajia kufanya mabadiliko Old Trafford. ***(Mirror)***

### MANE KUMRITHI LEWANDOWSKI

MSHAMBULIAJI wa Liverpool na Senegal, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30, atakuwa akifuatiliwa na Bayern Munich ikiwa mshambuliaji wao wa kimataifa wa Poland, Robert Lewandowski ataondoka msimu huu wa majira ya joto. ***(Bild)***

### DEMBELE AWINDWA BAYERN

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24, yupo kwenye orodha ya wachezaji wanaolengwa na Bayern Munich. ***(Sky Sports)***

### DE JONG KUONDOKA BARCA

KIUNGO wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong mwenye umri wa miaka 25, yuko tayari kuondoa klabuni hapo. ***(Sun)***

### LEWIN AITAKA ARSENAL

KLABU ya Newcastle imefanya mazungumzo ya awali na mshambuliaji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 25, lakini yeye mwenyewe anaitaka Arsenal. ***(Football Insider)***

### POGBA KURUDI JUVE

KLABU ya Juventus iko tayari kumrejesha kiungo wa kati wa Manchester United, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 29, katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto. Mkataba wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa unamalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Goal)***

### MAN CITY KUSAJILI ZAIDI

KLABU ya Manchester City itatafuta wachezaji zaidi wa kusajili baada ya kuwasili kwa mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Norway, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 21. ***(Mail)***

### HAALAND NA EVERTON

EVERTON walikataa fursa ya kumsajili Erling Haaland kwa pauni 60,000 mwaka 2016. ***(Times)***

### HICKEY ANUKIA ARSENAL

ARSENAL wamekubali ada ya hadi euro milioni 25 kwa beki wa pembeni wa kimataifa wa Bologna na Scotland, Aaron Hickey. ***(Calciomercato)***

### SAMUEL AGOMBEWA EPL

KLABU za West Ham, Southampton na Brentford zinavutiwa na beki wa kulia wa Fenerbahce, Bright Osayi-Samuel mwenye umri wa miaka 24. ***(Football Insider)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# KLOPP: SIWEZI KUJIVUNIA KUBEBA KOMBE LA FA

Nisingeweza, zaidi vijana wangu, jinsi walivyopambana, ulikuwa mchezo wa ajabu, mikwaju ya...

**LONDON,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema "hawezi kujivunia" timu yake inayowinda mataji manne baada ya kuishinda Chelsea kwa mikwaju ya penalti na kubeba Kombe la FA.

**Wekundu hao walisawazisha ushindi wao wa mikwaju ya penalti dhidi ya Chelsea kwenye fainali ya Kombe la Carabao kwa kushinda 6-5 baada ya dakika 90 za suluhu na muda wa nyongeza.**

"Nisingeweza kujivunia zaidi vijana wangu, jinsi walivyopambana," alisema Klopp akiiambia BBC Sport.

"Ulikuwa mchezo wa ajabu, mikwaju ya ujasiri."

Klopp mwenye umri wa miaka 54, amekuwa kocha wa kwanza wa Ujerumani kunyanyua Kombe la FA baada ya kumshinda Mjerumani mwenzake, Thomas Tuchel katika mchezo wa fainali uliopigwa Uwanja wa Wembley kwa mara ya pili katika muda wa chini ya miezi mitatu.

Kama ilivyokuwa katika fainali ya Februari, Alisson aliokoa penalti ya Mason Mount na kuipa Liverpool faida kabla ya Konstantinos Tsimikas kupachika penalti ya ushindi.

"Ilikuwa kali - Chelsea ingestahili kama vile tulivyostahili, kama tu katika Kombe la Carabao - ndivyo walivyo," aliongeza Klopp.

"Chelsea walicheza vema, lakini mwisho lazima kuwe na mshindi mmoja na ndio tulikuwa sisi leo (juzi)."

Ushindi huo wa kushangaza uliweka hai matumaini madogo ya Liverpool kubeba mataji manne ingawa taji la Ligi Kuu ya England linaweza kuwaepusha - zikiwa zimesalia mechi mbili na wakipitwa na vinara Manchester City kwa pointi tatu.

Kombe la FA ni kombe la sita kwa Klopp kushinda kama kocha wa Liverpool, akiwa tayari kabeba taji la Ligi Kuu, Kombe la Carabao, Ligi ya Mabingwa Ulaya, Uefa Super na Klabu Bingwa Dunia.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
NEWCASTLE
VERSUS
ARSENAL
1 | 3.83
X | 3.50
2 | 1.88

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# LEWANDOWSKI ATHIBITISHA KUONDOKA BAYERN MUNICH



**MUNICH,** Ujerumani

NYOTA wa Bayern Munich, Robert Lewandowski amethibitisha nia yake ya kuondoka klabuni hapo msimu huu wa majira ya joto.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland, amekuwa kwenye vichwa vya habari za uhamisho juu ya uwezekano wa kuongezwa mkataba pale Allianz Arena huku wa sasa ukikamilika mwishoni mwa msimu wa 2022/23.

Lewandowski anadaiwa kuwa anataka changamoto mpya, na nyota huyo anafikia umri wa miaka 34 Agosti mwaka huu, akiwa amecheza zaidi ya muongo mmoja wa soka nchini Ujerumani, huku Barcelona wakimfuatilia.

Awali, Bayern walikuwa wanatarajiwa kuongeza mkataba na Lewandowski, kuhakikisha wanasalia na nyota huyo wa zamani wa Borussia Dortmund.

Hata hivyo, kwa mujibu wa ripoti kutoka Sky Sport, Lewandowski sasa amewaambia viongozi wa klabu kuwa anataka kuondoka mwezi ujao, na anatajwa kuwa hana mpango wa kusubiri mkataba wake kumalizika.



## Tuchel: Sijutii Chelsea kupoteza Kombe la FA

**LONDON,** England

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel, amesema "hajutii" matokeo ya timu yake kwenye fainali ya Kombe la FA dhidi ya Liverpool baada ya kufungwa.

'The Blues' hao walifungwa na kikosi cha kocha Jurgen Klopp kwa mara ya pili pale Wembley - wakiwa pia wamepoteza fainali ya Kombe la EFL Februari - na tena ilikuwa kwa mikwaju ya penalti.

Ilikuwa ni mchuano mwingine mkali kati ya Chelsea na Liverpool, wakiwa wametoka sare katika mechi zote mbili za ligi msimu huu, lakini Tuchel hakuwa katika hali ya kujutia hilo kwa kukosa kombe mbele ya Mjerumani mwenzake.

"Kama katika fainali iliyopita, hakuna majuto," alisema Tuchel kocha wa zamani wa Borussia Dortmund na Paris Saint-Germain mara baada ya mchezo huo.





# NYOTA AZAM KUTIBIWA GOTI AFRIKA KUSINI

**Na Shufaa Lyimo**

MCHEZAJI wa Klabu ya Azam FC, Paul Peter, anatarajiwa kupelekwa Afrika Kusini kesho, Jumanne kutibiwa goti baada ya kuumia mazoezini, imeelezwa.

Akizungumza jijini jana Msemaji wa klabu hiyo, Thabit Zakaria 'Zaka Zakazi' alisema wachezaji wengine ambao walikuwa majeruhi Shabani Chilunda, Idd Nado tayari wameanza mazoezi mepesi.

"Mchezaji wetu Peter muda wowote anatarajiwa kuelekea nchini Afrika Kusini kufanyiwa matibabu, kwa upande wa majeruhi wengine wanaendelea vizuri," alisema Zaka Zakazi.

Kuhusu maandalizi ya mchezo wao ujao wa Ligi Kuu Bara keshokutwa, Jumatano dhidi ya Simba, alisema wamejipanga vizuri kuhakikisha wanaibuka na pointi zote tatu.

"Timu inaendelea na mazoezi kwa ajili ya kujiandaa kukutana na Simba hapo Mei 18, mwaka huu (Jumatano) ni mchezo ambao unatarajiwa kuwa na ushindani mkubwa," alisema.

Alisema Kocha wao, Abdihamid Moallin, anaendelea kuyafanyia kazi makosa yaliyojitokeza katika mchezo uliopita ili yasijirudie katika mchezo dhidi ya Simba.

Mchezo uliopita timu hiyo ilipoteza ugenini kwa kukubali kupokea kichapo cha mabao 2-1 dhidi ya Mbeya City katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya.

Azam FC ipo nafasi ya tatu ikiwa na pointi 32 wakati Simba ikiwa nafasi ya pili na alama zake 49, nane nyuma ya vinara Yanga kabla ya mechi za jana.

# *Ihefu yarejea tena Ligi Kuu Bara*

**Na Adam Fungamwango**

BAO lililofungwa dakika ya 68 na Issa Ngoah, limeirejesha Ihefu kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, kwa kuichapa timu kongwe ya Pan African bao 1-0 juzi kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali, Mbeya, kwenye mchezo wa Ligi ya Championship.

Haikuwa rahisi kwa Ihefu ambayo ilipanda na kucheza ligi msimu mmoja tu na kuteremka daraja msimu wa 2019/20, kwani ikicheza kwenye uwanja wake wa nyumbani, nyuma ya mashabiki wengi waliojazana kuishangilia kwa nguvu, ilibidi isubiri hadi dakika hiyo kupachika bao hilo pekee dhidi ya Mabingwa wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania mwaka 1982.

Timu hiyo imeungana na DTB FC kupanda Ligi Kuu moja kwa moja, lakini ikibakisha mchezo mmoja ili kumaliza mechi 30 za msimu.

Imetinga Ligi Kuu kwa kufikisha jumla ya pointi 65, ikicheza mechi 29, ikishinda 21, sare mbili, ikipoteza mechi sita, mabao 49 ya kufunga, ikiruhusu nyavu zake kuguswa mara 19. Kwa sasa inazidiwa pointi moja tu na DTB ambayo tayari nayo imepanda Ligi Kuu kwa mara ya kwanza.

Timu hiyo inayofundishwa na mchezaji na kocha wa zamani wa Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, itaongeza idadi ya timu kutoka Mbeya, ambazo baadhi yao kama Tanzania Prisons na Mbeya Kwanza zinasuasua kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Kutokana na msimamo jinsi ulivyo, timu mbili kati ya tatu, ambazo ni Kitayosce yenye pointi 58, JKT Tanzania 50 na KenGold 48, kila timu ikiwa imebakisha mechi moja, zitacheza mechi ya mchujo kupata mshindi ambaye atakwenda kucheza na timu iliyoshinda mechi ya mchujo Ligi Kuu, kusaka timu nyingine moja itakayocheza Ligi Kuu msimu wa 2022/23.


CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 16/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2659 | Ruvu Shooting vs KMC | 2.37 | 2.77 | 3.16 |
| 16:00 | 1996 | Merani Martvili vs FC Norchi Dinamo Tbilisi | 1.53 | 4.00 | 5.07 |
| 16:00 | 2771 | Spartak II Moscow vs KamAZ | 2.35 | 3.06 | 2.87 |
| 16:00 | 2787 | Tanzania Prisons vs Kagera Sugar | 2.67 | 2.62 | 2.91 |
| 17:00 | 2252 | Otmk Olmaliq vs Bunyodkor | 1.90 | 3.05 | 4.07 |
| 17:00 | 3582 | FC Olimpik vs Lokomotiv Tashkent | 4.86 | 3.01 | 1.78 |
| 18:30 | 2561 | NK Osijek II vs Kustosija | 2.88 | 3.02 | 2.37 |
| 18:30 | 3182 | Luka Koper vs NK Radomlje | 1.47 | 4.15 | 5.60 |
| 19:00 | 1244 | Viking vs Jerv | 1.21 | 6.18 | 11.96 |
| 19:00 | 1784 | AEL Limassol vs Doxa Katokopia | 2.03 | 3.39 | 3.54 |
| 19:00 | 1861 | Odd Ballklubb vs Haugesund | 2.10 | 3.44 | 3.24 |
| 19:00 | 1906 | Brann vs Sandnes Ulf | 1.40 | 4.47 | 6.21 |
| 19:00 | 1992 | Stabaek vs Grorud IL | 1.45 | 4.28 | 5.65 |
| 19:00 | 2278 | FC Elva vs Viimsi JK | 2.21 | 4.19 | 2.64 |
| 19:00 | 2587 | Follo vs Start 2 | 1.79 | 4.27 | 3.25 |
| 19:00 | 2961 | Moss-Orn vs Horten | 1.70 | 3.91 | 3.91 |
| 19:00 | 3115 | Bodo Glimt vs Tromso | 1.45 | 4.57 | 5.97 |
| 19:00 | 3630 | Rosenborg vs Sandefjord | 1.48 | 4.38 | 5.78 |
| 19:00 | 3954 | FC Carlos Stein vs Atletico Grau | 2.42 | 3.06 | 2.77 |
| 19:00 | 4035 | Aalesunds vs Molde | 3.19 | 3.53 | 2.09 |
| 19:00 | 4114 | Olympiakos Nicosia vs Ethnikos Achnas | 1.94 | 3.35 | 3.90 |
| 19:00 | 4955 | Kristiansund vs Stromsgodset | 2.20 | 3.38 | 3.08 |
| 19:00 | 5072 | Fredrikstad vs Skeid Fotball | 1.52 | 4.27 | 4.86 |
| 19:00 | 5515 | Sitra Club vs Malkiya Club | 1.43 | 4.47 | 5.64 |
| 19:00 | 5883 | Lillestrom vs Sarpsborg | 1.90 | 3.53 | 3.78 |
| 19:00 | 5989 | Floro vs Forde | 2.71 | 3.97 | 2.08 |
| 19:30 | 2228 | Ghazl EL Mahallah vs Eastern Company SC | 1.85 | 3.00 | 4.99 |
| 19:30 | 3895 | Sampdoria vs Fiorentina | 4.06 | 3.71 | 1.77 |
| 20:00 | 1630 | Caykur Rizespor vs Sivasspor | 2.75 | 3.29 | 2.46 |
| 20:00 | 2244 | Silkeborg vs Midtjylland | 2.60 | 3.45 | 2.50 |
| 20:00 | 2299 | IK Oddevold vs Ljungskille | 2.04 | 3.85 | 3.15 |
| 20:00 | 4731 | Galatasaray vs Adana Demirspor | 1.93 | 3.69 | 3.49 |
| 20:10 | 4123 | Djurgardens IF vs Malmo | 2.33 | 3.16 | 2.82 |
| 20:30 | 2585 | U Craiova SA vs Sepsi Osk | 3.37 | 3.02 | 2.21 |
| 20:30 | 2847 | Maccabi Tel Aviv vs Hapoel Beer Sheva | 2.17 | 3.21 | 3.06 |
| 20:30 | 3013 | CS Mioveni vs Rapid Bucuresti | 5.36 | 3.37 | 1.68 |
| 20:30 | 3081 | Clinceni vs Botosani | 21.76 | 8.11 | 1.10 |
| 20:30 | 4429 | Bnei Sakhnin vs Maccabi Haifa | 7.21 | 4.38 | 1.36 |
| 20:30 | 5143 | Maccabi Netanya vs Hapoel Tel Aviv | 1.98 | 3.31 | 3.41 |
| 21:00 | 1538 | FC Ajka vs Diosgyori Vtk | 4.19 | 3.41 | 1.76 |
| 21:00 | 3475 | Valerenga vs Ham-Kam | 1.66 | 3.84 | 4.68 |
| 21:45 | 1302 | Juventus vs Lazio | 2.35 | 3.36 | 2.79 |
| 21:45 | 1724 | Huddersfield vs Luton Town | 2.21 | 3.12 | 3.27 |
| 21:45 | 4352 | Treaty United vs Longford Town | 2.76 | 3.20 | 2.35 |
| 22:00 | 2509 | Real Oviedo vs Zaragoza | 1.59 | 3.62 | 5.75 |
| 22:00 | 5007 | Newcastle vs Arsenal | 3.83 | 3.50 | 1.88 |
| 22:00 | 5590 | Smouha Club vs Al Masry Club | 2.19 | 2.78 | 3.87 |
| 22:15 | 2172 | Vikingur Reykjavik vs Breidablik | 2.77 | 3.55 | 2.19 |
| 22:15 | 2309 | Leiknir vs Fram Reykjavik | 2.03 | 3.50 | 3.11 |
| 22:15 | 4704 | KR Reykjavik vs Keflavik IF | 1.38 | 4.66 | 6.22 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumatatu Mei 16, 2022

Nipashe



Klopp: Siwezi kujivunia Kombe la FA UKURASA 21

**'NO KUTETEMA'...**



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akiruka kujaribu kufunga kwa kichwa, huku Kipa wa Dodoma Jiji, Mohamed Yusuph, akimfuata juu kwa juu kuokoa katika mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma jana na kumalizika kwa wageni kushinda mabao 2-0. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Yanga yaamka mbio ubingwa*

## ●●● Ambundo aiongoza kuicharaza Dodoma Jiji, Mayele akishindwa tena kutetema...

**Na Adam Fungamwango**

VINARA wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, jana walihitimisha ukame wake kucheza mechi tatu sawa na dakika 270 bila kupata bao lolote, walipoiadhibu Dodoma Jiji mabao 2-0 kwenye mechi ya raundi ya 24 ya Ligi Kuu Tanzania Bara na kuukaribia ubingwa ambao imeukosa kwa misimu mitatu sasa.

**Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma, straika wa timu hiyo, anayeongoza kwenye mbio za ufungaji bora, Mkongomani Fiston Mayele akiwa na mabao 12, sawa na George Mpole wa Geita Gold FC alifikisha mechi ya nne mfululizo bila kufunga bao lolote, Kocha Mkuu Nasreddine Nabi akilazimika kumtoa dakika mbili kabla ya mechi kumalizika na kuingia, Heritier Makambo.**

Mayele hakufunga mechi dhidi ya Simba, Ruvu Shooting, Prisons na ya jana dhidi ya Dodoma Jiji. Kwenye mechi hiyo, Yanga ilipata mabao yake yote kipindi cha kwanza kupitia kwa Dickson Ambundo aliyefunga bao la kwanza dakika ya 11, akiwaadhibu waajiri wake wa zamani kwa shuti kali la mbali, umbali wa takribani mita zitapazo 25 hivi.

Ilikuwa ni pasi ya Jesus Moloko ambaye aliuhamisha mpira kutoka upande wa mashariki mwa uwanja kwenda magharibi, ukamkuta mfungaji akiwa hajakabwa na mtu yeyote, bila kuchelewa akifumua 'mashine' iliyokwenda moja kwa moja nyavuni, huku kipa Mohamed Yusuph akiambulia kuutazama tu.

Ambundo ambaye kama angekuwa makini angeweza kufunga 'hat-trick' na kuondoka na mpira wake, hakushangilia akionyesha mapenzi kwa timu yake hiyo ya zamani kabla ya kutua Yanga.

Dodoma ingeweza kusawazisha dakika nne baadaye, lakini straika wake Anuary Jabir aliyeonekana kuwa msumbufu kwa mabeki wa Yanga, akiwa yeye na lango akapiga juu. Mayele aliyewekwa chini ya ulinzi na Gerald Mgeveke na Augustine Nsata, aliikosesha Yanga bao, alipopiga kichwa juu, akiunganisha krosi ya Kibwana Shomari.

Anuary tena, nusura aifungie Dodoma Jiji bao dakika ya 30, baada ya kuletewa mpira na Kibwana, aliyekosea kuuokoa, lakini kichwa alichopiga kilitoka nje ya lango la Yanga. Dakika ya 35, Yanga ikiandika bao la pili lililofungwa kutokana na shuti kali la mbali lililopigwa na Zawadi Mauya, ambao kipa Yusuph alijaribu kuuokoa, ukimponyoka mara tatu mikononi kabla ya kutinga wavuni, likihesabiwa ni bao la kujifunga.

Baada ya kushuhudiwa mpira wa kasi na pasi ndefu kutoka kwa timu zote mbili, kipindi cha pili hakikuwa kama cha kwanza, kwani kasi ilionekana kupungua hasa kwa Yanga, huku Dodoma Jiji wakipambana kusaka mabao ya kusawazisha, lakini umakini wa wachezaji wake kina Waziri Shentembo, Emmanuel Martin na Anuary haukuwapo.

Kipa Djugui Diarra alilazimika kufanya kazi ya ziada, dakika ya 69 na 70, baada ya mashambulizi makali yaliyoelekezwa langoni mwake.

Ilikuwa ni faulo iliyopigwa na Martin, lililowababatiza wachezaji wa timu zote mbili na kumkuta, Waziri ambaye alibetua kutaka kuukwamisha wavuni, lakini Diarra aliuokoa ustadi na kuwa kona ambayo nayo ilileta kizaazaa nusura izae bao, lakini pia aliisalimisha timu yake.

Denis Nkane aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Jesus Moloko, alikosa bao yeye na wavu dakika ya 80, baada ya kupiga shuti kali lililogonga nguzo ya pembeni huku kipa Yusuph akiwa hayupo golini.

Yanga sasa inafikisha pointi 60 kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu, ikiiacha Dodoma Jiji kwenye nafasi ya nane ikiwa na alama zake 28, lakini vinara hao wa ligi wakiweka pengo la pointi 11 baina yake na anayeshika nafasi ya pili mabingwa watetezi, Simba.

## Pablo: Yanga haikustahili FA

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesema mechi ya nusu fainali timu yake ilipaswa kucheza na Geita Gold FC na si Yanga kwa sababu hawakustahili, lakini amejipanga kushinda mchezo huo.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi ya robo fainali ya Kombe la FA kati ya timu hiyo na Pamba FC juzi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam na kupata ushindi wa mabao 4-0, kocha huyo alisema anachofahamu ni kwamba Geita Gold ndiyo ilistahili kuicheza hatua hiyo.

"Sifurahii kukutana na Yanga katika hatua inayofuata kwa sababu hakustahili, ningekutana na Geita Gold ingekuwa vizuri zaidi kwa maana ndiyo waliostahili, lakini hata hivyo tumejipanga kucheza na kushinda," alisema kocha huyo raia wa Hispania.

Akizungumzia mechi dhidi ya Pamba, alisema pamoja na kukosa mabao mengi, wachezaji wake mwanzo hawakuonekana kucheza kwa kujituma kwa sababu walikuwa wanacheza na timu ambayo ipo kwenye daraja la chini.

"Tungeweza kufunga mabao matano ndani ya dakika 15 tu, nisingeweza kufanya chochote kama wachezaji wanafanya kila kitu, lakini wanashindwa tu kuweka mpira wavuni, niliongea nao wakati wa mapumziko, kwa kiasi fulani walibadilika kipindi cha pili," alisema Pablo.

Yalikuwa ni mabao mawili ya Yusuph Mhilu, Peter Banda na Denis Kibu yaliyoiwezesha timu hiyo kutinga hatua hiyo. Kaimu Kocha Mkuu wa timu ya Pamba, Steven Matata, alisema timu yake haikustahili kuingia nusu fainali mbele ya Simba.

Alisema aina ya wachezaji wake na uwezo wa Simba ni vitu viwili tofauti kwani walizidiwa ufundi, ujanja, ukomavu na uzoefu.

"Kwangu mimi ulikuwa ni mchezo wa fahari wa kujivunia timu yangu na vijana wangu kucheza na timu ya Simba, yote yaliyofanyika uwanjani ni kwamba vijana wamejitahidi, tumezidiwa ujanja, uzoefu, ufundi na ukomavu," alisema.

Hii itakuwa ni mara ya tatu kwa Simba na Yanga kukutana kwenye michuano ya Kombe la FA kwa misimu mitatu mfululizo. Yanga iliingia hatua hiyo kwa kuitwanga Geita Gold kwa mikwaju ya penalti 7-6, baada ya sare ya bao 1-1.

Misimu miwili iliyopita zilikutana hatua ya nusu fainali Julai 12, 2020, Uwanja wa Banjamin Mkapa, Simba ikishinda mabao 4-1 na mara ya pili ni msimu uliopita zilipocheza fainali kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma Julai 25, 2021, Simba ikishinda tena bao 1-0.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >